# Sikukuu Ya Baragumu

Jeffersonville, Indiana, USA

Julai 19, 1965A

1 Na tuinamishe vichwa vyetu. Bwana, wakati mmoja ilisemwa, na wanafunzi Wako wapendwa, "Tufundishe kuomba." Kwa kuwa tunapomwona Mungu mkuu wa Mbinguni, tunatambua jinsi tulivyo duni. Kwa hiyo tufundishe kuomba, Bwana, mioyoni mwetu sasa, kwa ajili ya mambo ambayo—ambayo yatafaidi Ufalme Wako na kwa ajili ya watumishi Wako. Wewe unajua haja ya kila mtu hapa.

Na hapa kwenye dawati, asubuhi ya leo, kuna leso na vitambaa, na vifurushi vidogo tu kutoka kwa wahitaji wa msaada wa kimwili, na wa nyumbani, na cho chote kile. Lakini Wewe ni Mungu, na Mungu peke yako, Mungu wa pekee wa kweli aliyeko. Nasi tunakuomba katika Jina la Yesu, Mwanao mpendwa, ya kwamba utamponya kila mmoja wa hawa. Na huenda kukawa na wengine hapa ambao hawana leso hapa, wala kifurushi, wanaohitaji uponyaji.

Huenda kukawa na baadhi ya watu kote ulimwenguni, kote ulimwenguni, ambao hata kanda hii wangekutana nayo majumbani mwao ama makanisani mwao. Tungeomba, Bwana, kwamba wakati ibada inaendelea, pale—pale…au kanda inachezwa, au nafasi yo yote tunayoweza kuwamo, au—au hali, yule Mungu mkuu wa Mbinguni na aheshimu huu unyofu wa mioyo yetu asubuhi hii, na kuponya wahitaji, kuwapa wao yale wanayohitaji.

Tubariki sasa katika ibada ijayo. Nena kupitia sisi, kwa namna haijawahi kutokea, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Tunangojea, katika Jina la Yesu, kwa ajili ya jibu Lako. Amina.

Utanisaidia kwa hili? [Ndugu Branham anaondoa vitu mimbarani — Mh.]

2 Ni vizuri kuwa hapa kanisani tena asubuhi ya leo. Nami nilikuwa nikizungumza tu na marafiki ambao ndio kwanza waje kutoka Ohio, kwa msichana mdogo, ambaye aliletwa hapa miezi michache iliyopita, aliyekuwa anakufa kwa lukemia. Watu walikuwa maskini sana, wale wazazi. Nami sina nafasi asubuhi hii kusoma ule—ule ushuhuda ambao utawekwa katika faili. Lakini kuna hiyo picha ya msichana huyo mdogo baada ya siku tatu, naamini ilikuwa, baada ya kuombewa. Madaktari walimpa siku tatu tu za kuishi, na katika siku tatu baadaye hawakuweza hata kupata dalili yake. Na kwa hiyo yuko shuleni, mwenye furaha sana. Nina hakika kanisa linakumbuka tulipokuwa naye hapa chumbani.

Na pia mtoto mchanga aliyezaliwa na matumbo, kama, nje. Kwa namna fulani wale madaktari, na hii hali dhaifu ya jinsi matumbo yalivyoumbika, yasingeweza kurudishwa tena. Waliogopa kugusa kitu hicho kidogo, ni mtoto mchanga tu aliyezaliwa. Na sasa, jamaa huyo mdogo ana umri wa karibu mwaka mmoja, nadhani, kitu kama hicho, akiwa na matumbo ya kawaida, kila kitu ni cha kawaida tu awezavyo kuwa. Ni neema tu ya Mungu, kwamba jinsi alivyo mwema kwetu.

3 Sasa, leo, nilikuwa nataka kutangaza ya kwamba mkutano tuliokuwa tukipanga, nilikuwa nikipanga kwenda kwenye juma hili lijalo huko—huko Afrika, huku pamoja na Ndugu Joseph Boze, huko Kenya na Tanganyika. Hatuwezi kuwa na mkutano, tukiwa na telegramu kutoka kwa Ndugu Boze, "Wiki iliyopita wamishenari wetu watatu walipatwa na mauti, waliuawa."

Nao wana maasi kule sasa. Na wakomunisti wanapenyeza bunduki kwa wenyeji, wakidai wanazo mashua za kuvulia zimeegeshwa kote, China na Urusi; na wakiwapa bunduki wenyeji, nao hawajui kuzitumia vema kuliko kuzitumia kwa kitu cho chote tu wanachokiona. Kwa hiyo, hapo, ile—ile—ile serikali ilidhani ya kwamba isingekuwa jambo la hekima kufanya mkutano wakati huu. Na kama ninavyofahamu, pia, ya kwamba Ndugu Boze hawezi hata kufungua shule yake katika eneo hili, mahali nilipokuwa nikienda, wakati huu. Lakini haukufutiliwa mbali, umeahirishwa tu hadi wakati watakapoweza kutuliza jambo hilo tena.

4 Nina furaha sana asubuhi ya leo kuona, katikati yetu tena, kwa miaka mingi bila kuwepo, Ndugu Jackson, Ndugu Sidney Jackson na Dada Jackson, kutoka Afrika Kusini. Wamezungumza? [Ndugu Neville anasema, "Ndiyo" — Mh.] Na watu hawa walikuwa ni ndugu na dada zangu halisi, na wafanyakazi wenzangu katika kampeni huko Afrika Kusini, safari ya mwisho kule. Ambapo, tunaamini ya kwamba siku moja, kwa neema ya Mungu, kurudi pamoja nao tena, kwa kuwa ni mhitaji.

Nami nimekuwa nikijaribu kwa miaka tisa kurudi. Lakini, kwa sababu ya madhehebu, na kadhalika, hawataniruhusu kurudi. Kwa hiyo niliwaandikia barua hivi karibuni, na kusema, "Basi damu ya hao watu waliopotea na iwe juu yenu wala si juu yangu." Kwa kuwa, ninaamini ya kwamba Mungu alikuwa akitaka kutumia huduma yangu kule, kwa ajili ya watu hao, kwa wakati fulani. Na kwa tofauti yao ya kimadhehebu, hawataniruhusu kurudi. Lakini, vema, Bwana atashughulikia jambo hilo.

5 Sasa, yale ninayotaka kusema asubuhi ya leo, ya kwamba Bwana akipenda, Ndugu Neville ameniomba kuwa na ibada usiku wa leo, na kwenye Maskani. Kwa hiyo sisi … Umealikwa utoke. Na halafu Jumapili ijayo, Bwana akipenda, nitakuwa hapa, pia; halafu labda kwa Jumapili mbili ama tatu zijazo, kwa sababu ya kutokuwepo kwa jambo hili, kwa kuwa ni kufutiliwa mbali kwa mkutano huu uliokuwa unafanywa.

6 Sasa, sisi pia tungependa kusema, ya kwamba, nilisema labda tungehubiri zile Baragumu Saba katika wakati huu. Hatukujua tu jinsi gani tungepata kutenda hili katika ufinyu wa nafasi katika jengo na kukosekana kwa kiyoyozi, hakuna hewa katika chumba. Hakijatayarishwa bado kwa viyoyozi. Nasi tulijaribu kukodisha shule hii hapa juu, ambayo ina viyoyozi, ambayo imekaa yapata … Loo, sijui; ni nafasi nzuri ya kuketi, shule nzuri sana. Lakini hatungepata kitu.

Na, ingekuwa, wangetupa juma lijalo. Lakini, juma lijalo? Mnaona, kuna wajumbe wanaokuja kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu; kutoka Jamaica, na kutoka Visiwani, na kutoka kusini, hata katika Amerika ya Kusini, na Canada, na Mexico, na kote nchini. Nasi tulituma taarifa Jumatatu, basi hawangezipata mpaka Jumatano ama Alhamisi; halafu inawabidi kuomba muda wa mapumziko, na kadhalika, ambao ungetupilia hili mbali.

Majuma yafuatayo, kuendelea, mpaka wakati wa shule, ni, ingepasa kuchukua usiku mmoja, na kisha kupumzika kwa usiku mmoja au mbili, kisha kuendelea tena, halafu… Tusingeweza kufanya hivyo. Usingeweza kufanikiwa.

7 Nilishangaa ni kwa nini, wakati nilikuwa nimeomba kwa uaminifu. Na basi ni karibu wakati wetu wa kurudi Arizona tena, kwa watoto kuingia shuleni. Na halafu sisi … Nilikuwa nikizungumza na mke wangu.

Na, vema, jana niliingia chumbani, na nikasema, "Bwana, na—huenda nisitumie maneno mengi sana, lakini, elewa, tafadhali, Mungu, kile ninachomaanisha moyoni mwangu. Kuna nini kwamba kila kitu kimekatiliwa mbali kuhubiri hizo Baragumu?" Na ndipo akaja na kulifunua. Na sasa, asubuhi ya leo, ninataka kuzungumza nanyi juu ya sababu yake.

Na sasa hebu sisi, ambao tuna Biblia na tungependa ku—ku, tufungue Biblia zetu. Tutafungua kwanza kwenye Mambo ya Walawi, mlango wa 23 wa Mambo ya Walawi.

Kama Bwana akipenda, usiku wa leo nitahubiri juu ya somo: *Kuenda Nje Ya Kambi*. Na itakuwa ni fupi, na kwa hiyo unaweza kuwa na wakati wa kurudi mahali pako kazini.

8 Tuna furaha kuona wageni wameingia, watu kutoka nje ya mji. Ni watu wangapi walio nje ya mji walio hapa, tunapoangalia? Asilimia tisini na tano, naam, asilimia tisini na nane ya kusanyiko. Kwa hiyo, mnaona si Jeffersonville, ni watu wanaokuja Jeffersonville, wanaofanya … Tuko hapa kwa neema ya Bwana.

Na sasa ninataka kusoma sehemu tatu, asubuhi ya leo. Moja ya hizo inapatikana katika Mambo ya Walawi sura ya 23, na hiyo nyingine ni katika Isaya 18, na Isaya 27, ninyi mnaoandika.

Na sasa badala ya kuhubiri … Bwana akipenda, nitafanya hivyo usiku wa leo. Lakini ninataka kufundisha, asubuhi ya leo, juu ya sikukuu ya zile baragumu saba. Ambapo, mwezi huu ni sikukuu ya baragumu saba, kuanzia … na ambao ni mwezi wa saba, ambao ungekuwa Julai 15, ulikuwa mwanzo wa sikukuu ya baragumu, katika sheria za Walawi.

9 Sasa, na kama mna karatasi zenu na kadhalika, na mnataka kuandika Maandiko na vifungu vya masomo, na kadhalika, tunapoendelea mbele.

Kuna jambo moja kwa mkutano huu, ni joto, nasi tumezoea hilo miaka mingi. Bali mtu fulani anaweza kufikiri kwamba naamini kwamba wakati tunapoingia katika hili jengo kwamba tunakomesha wakati, huenda ikawa, kwa sehemu, kwa sehemu tuko katika Umilele, kwa jinsi ya muda mrefu ninaowaweka watu. Simaanishi iwe hivyo. Lakini ninaamini ya kwamba tunaishi karibu sana na kule Kuja kwa Yesu, hata inanibidi kutumia kila dakika ambayo ninawaweka watu pamoja.

Nami nilikuwa nikiwazia, nilipokuwa nikiendesha gari barabarani muda mfupi uliopita, nikiwa huko nje kwa ajili ya maombi madogo kabla tu ya kuingia mimbarani, kama kasisi ye yote mwaminifu anavyofanya. Nilikuwa nikiwaza, "Unajua, tunakuwa na wakati mzuri sana tunapokutana hapa pamoja! Lakini, na watu wanaokusanyika kutoka katika majimbo mengi, wameketi papa hapa sasa, kutoka mbali sana, mamia na mamia ya maili, nasi tunakusanyika pamoja kushiriki katika Neno. Lakini utakuja wakati, hivi karibuni, ambapo huu utakuwa ni kumbukumbu nzuri." Hiyo ni kweli.

Nyakati hizi zitaondolewa kwetu, kwa hiyo basi hatuna budi kufanya yote tunayojua jinsi ya kufanya, kuifanya hii, kila dakika, ihesabiwe. Na wazia jambo hili sasa, tunapoteseka katika joto la asubuhi. Na, mnajua, kila mwili wa mwanadamu ni—ni mtambo wa joto, wenyewe, na hilo linafanya kuwa gumu sana kwako. Na, lakini ninawatakeni mpate Neno.

Sasa, kabla tu ya sisi—sisi kusoma, hebu tuombe.

10 Bwana, karibu kila mtu humu ambao wanaweza kusogeza mikono yao, wangeweza kugeuza kurasa za Biblia hii. Lakini kuna Mmoja tu miongoni mwetu asubuhi hii anayeweza kuifungua; Huyo ni yule Roho Mtakatifu aliye mkuu, aliye katikati yetu. Tufunulie Neno, Bwana, tunaposoma, kama ulivyowafanyia wanafunzi, walipokuwa wakienda zao Emau, na kuanza kuwaelezea Maandiko. Na jalia sisi, tutakapoondoka, tuseme kama wale waliorudi Yerusalemu kutoka Emau, "Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani

yetu alipokuwa akisema nasi njiani?" Kwa kuwa ni katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

Hebu na tusimame katika kuheshimu Neno.

11 Sasa, somo langu asubuhi ya leo ni: *Sikukuu ya Baragumu*. Ninataka kusoma sasa kutoka kwenye kifungu cha 23 cha sura ya 23 ya Mambo ya Walawi.

> *Kisha BWANA akanena na Musa, na kumwambia,*
>
> *Nena na wana wa Israeli, uwaambie, Mwezi wa saba, siku ya kwanza ya mwezi, kutakuwa na kustarehe kabisa kwenu, ni ukumbusho wa kuzipiga baragumu, ni kusanyiko takatifu.*

Sasa katika Kitabu cha Isaya, kuanzia kifungu cha 1 cha mlango wa 18, hili linaunganisha hili pamoja.

> *Ole wa nchi ya uvumi wa mabawa, Iliyoko mbali kupita mito ya Kushi!*
>
> *Ipelekayo wajumbe wake kwa njia ya bahari, na vile vyombo vya unyasi juu ya maji, na kusema, Nendeni, wajumbe wepesi, kwa taifa lililotawanyika…bambuka, kutoka kwa watu watishao…taifa lililolainishwa na kukanyagwa chini, ambao mto umeharibu nchi yao!*
>
> Na *ninyi watu mkaao katika ulimwengu wote, na wenyeji wa dunia, akiinua bendera mlimani, angalieni; na akipiga tarumbeta, sikieni.*

Katika Isaya 27:12 na 13.

> *Tena itakuwa katika siku hiyo, BWANA atayapiga-piga matunda yake toka gharika ya Mto hata kijito cha Misri, nanyi mtakusanywa mmoja mmoja, enyi wana wa Israeli.*
>
> *Tena itakuwa katika siku hiyo, tarumbeta kubwa itapigwa, nao waliokuwa karibu na kuangamia katika nchi ya Ashuru watakuja; na hao waliotupwa katika nchi ya Misri; nao watamsujudu BWANA katika mlima mtakatifu huko Yerusalemu.*

12 Hebu na tuombe tena. Bwana, bariki Maneno haya mioyoni mwetu. Jalia mawazo yetu na mawazo yetu yawe sawasawa na agizo Lako. Katika Jina la Yesu. Amina. Mnaweza kuketi.

13 Kuna mambo mengi sana ambayo mchungaji angetaka kusema kwa kusanyiko lake ambalo analipenda, la watu mbalimbali kutoka mahali mbalimbali, ambalo halingeruhusiwa kwa sababu ya wakati.

Sasa tunapokaribia somo hili, tunawataka mjisikie huru. Na wengi wenu wamesimama; na nilipokuwa nikipita, kumbi zilijaa, na nje ya milango, na mbele, na kuzunguka jengo, na kuzunguka kuta. Kwa hiyo, sasa, mkitaka kubadilishana viti ninyi kwa ninyi, hilo litakuwa sawa.

14 Sasa, *Sikukuu ya Baragumu*. Sasa, huu ulikuwa mkutano wa Israeli, ambapo walikusanyika pamoja, sikukuu ya baragumu.

Sasa, nimekuwa nikitarajia kwa muda fulani ku—kuzungumza juu ya somo la zile Baragumu Saba katika Kitabu cha Ufunuo. Na sasa tutarudia jambo hili, kwa muda kidogo tu, kuleta sababu halisi ya mimi kutozungumza wakati huu, kwa sababu Roho Mtakatifu asingeniruhusu kunena wakati huu juu ya mambo haya. Ninajua hilo linasikika kuwa ni la kitoto sana, labda, kwa watu wenye elimu na ufahamu mkubwa, lakini kwa Mkristo ni tofauti. Tu—tunafuata uongozi wa Roho, hilo peke yake.

15 Sasa, naanza kuona kwenye mahubiri ya Nyakati Saba za Kanisa, ambayo ni—ni mfano, au utabiri wa yote ambayo Mungu alikuwa anaenda kuyafanyia makanisa, na kupitia makanisa, na kuyaweka mahali pake.

Sura tatu za kwanza za Kitabu cha Ufunuo zinafunua matukio yote kwa Kanisa. Halafu, kutoka sura ya 3 hadi sura ya 19 ya Ufunuo, Kanisa halionekani tena. Kanisa linapanda juu kwenye mlango wa 4 wa Ufunuo, na linarudi kwenye sura ya 19 ya Ufunuo, Bibi-arusi na Bwana Arusi, pamoja, wakija duniani. Na halafu kutoka sura ya 19 hadi mwisho wa sura ya 22, yote yako kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu na ni kitu gani kitakachokuwa katika miaka itakayofuata. Katika sura ya 4 hadi 19, Mungu anashughulika na Israeli.

16 Sasa, basi, tulipomaliza na kitabu cha ufunuo wa kanisa, kile Mungu alichofanya kwa hayo makanisa saba, ambayo wakati huo yalikuwa katika uchanga wao, ama kivuli chao, huko Asia Ndogo. Ndipo Roho Mtakatifu alifunua na kufungua kwetu siri zote zilizomo Humo, za jinsi Yeye amelileta Kanisa Lake kupitia historia. Na kama huna Nyakati Saba za Kanisa katika kanda, ingekuwa vema kama ungezisikiza. Na hivi karibuni zitakuwa katika mfumo wa vitabu.

Halafu tu tukiacha hilo hapo, na kudhania ya kwamba baada ya kitambo kidogo tungehubiri juu ya ile Mihuri, bila kujua ile Mihuri ilikuwa ni nini.

Nilikuwa na wazo langu mwenyewe, kama kila mhudumu anavyofanya, la kusoma labda yale mtu mwingine aliyokuwa amesema; na kuamini kadiri niwezavyo, pamoja nao, juu ya mambo waliyokuwa wametoa, hitimisho lao. Nilikuwa nimesoma kitabu cha Bw.Smith, Uriah Smith, ambaye ni mwalimu wa Wasabato, nami nilikuwa nimesoma mawazo ya—yake juu hilo. Nami nilikuwa nimemsoma Bw.Larkin. Nilikuwa nimesoma, loo, vya wengi sana mbalimbali, kuhusu maelezo yao juu ya jambo Hili. Bali, kwa njia moja au nyingine, nilifikiri nilikuwa na—na ufahamu mdogo wa jambo hilo, mimi mwenyewe, ambao ungeweza kuwa tofauti mahali pengine. Lakini kujaribu wakati mmoja, nikinena tu masomo matatu, ya kwanza … ama masomo manne ya wale wapanda farasi wanne. Nilihubiri juu yake siku nne, mmoja juu ya farasi mmoja, na huyo mwingine.

17 Lakini basi kabla tu halijatukia, nilipewa ono, ambalo liko kwenye kanda, kama mjuavyo nyote, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* ya kwamba ninapaswa kwenda Tucson, Arizona. Na kule nyuma ya jangwa, huko juu mlimani, ambako nilikuwa pamoja na baadhi ya ndugu, na kuwaambia juu ya mlipuko mkuu utakavyotokea, nami … Malaika saba wakashuka. Mimi nikiwaza, mwenyewe, ulikuwa ni mwisho wa maisha yangu: nilimwambia mke wangu akae na Billy, na atakachofanya na hao watoto, na kadhalika, hata tutakapokutana tena nga'mbo ya pili.

18 Ndipo siku moja huko Sabino Canyon, wakati Mungu aliponiita asubuhi na mapema kule juu, nilikuwa nimeinua mikono yangu hewani, nikiomba, na upanga ukaingia mikononi mwangu. Unajua jambo hilo. Nilisimama pale na kuutazama, ni wa kawaida tu kama mkono wangu ulivyo sasa, bila kujua ulimaanisha nini. Nao uliachwa kwangu na Sauti iliyosema, "Huu ni ule Upanga wa Mfalme." Halafu basi, baadaye, wakati Malaika wa Bwana alipolifunua, lilikuwa ni Neno mkononi.

Mara tu baada ya hilo, Malaika wa Bwana walitokea na kuniambia kuhusu zile Baragumu Saba…au zile Muhuri Saba, kwamba ilikuwa nirudi hapa Jeffersonville na kuhubiri zile Muhuri Saba. Na, hapo, kama nimewahi kusema lo lote ambalo lilikuwa limevuviwa, ilikuwa katika hizo. Hapo ambapo Malaika wa Bwana alikutana nasi, na Biblia ikawa Biblia mpya. Hapo likafunguka na kufunua mambo yote ambayo watengenezaji na kadhalika walikuwa wameyaacha. Ulikuwa ni ule ufunuo mtimilifu wa Yesu Kristo, kwa jumla mpya kwetu, bali mkamilifu sawasawa kabisa na Maandiko. Hilo lilikuwa ni Neno ambalo limekuwa daima. Nilikuwa nimevuviwa sana na kuelekezwa.

19 Ndipo nilipokuja kwenye sehemu hii hapa, ya kuhubiri zile Baragumu Saba, nilikuwa nimewaza, "Vema, sitajaribu kuwazia jambo lo lote. Nitangojea tu mpaka wakati huo na kumwacha Yeye anifunulie." Na halafu jana wakati nilipokuwa … Niliingia chumbani na kushangaa ni kwa nini … Ama, samahani, ilikuwa ni juzi. Wakati nilipokwenda chumbani, kujaribu kuelewa, hapo ndipo Roho Mtakatifu alilifungua hili, kunionyesha mimi sababu gani jambo hilo hata halina manufaa kwa Kanisa kwa wakati huu, sababu halina uhusiano wo wote na Kanisa, kabisa.

20 Sasa, siri za Kristo zilizofichwa zilifunuliwa kikamilifu katika ile Mihuri Saba.

Ilifunua, kwanza, zile Nyakati Saba za Kanisa, ikafungua zile nyakati na kuziweka hizo mahali pake, kwa historia na kwa Biblia pia, na kuzipanga mahali, jinsi zilivyokuwa. Nasi tulijikuta katika wakati wa mwisho wa kanisa, tukiwa ni Wakati wa Kanisa la Laodikia, ambao ulikuwa ndio ulioharibika kuliko nyakati zote za kanisa. Hata kutoka lile la kwanza kabisa, kutoka Waefeso, ulikuwa wakati mkuu wa kanisa.

Na halafu jinsi ambavyo, hapa, Roho Mtakatifu akinipa ono, na kuona yale yangetukia, nilichora ubaoni, miaka miwili iliyopita. Hii hapa juu hapa kwenye mchoro, jinsi ambavyo ile Nuru ilikuwa ikififia katika duniani, ambapo ingekuwa sawasawa na vile Nuru ilivyokuja duniani, kama Injili, na jinsi itakavyofifia na kutoweka. Bila kujua jambo hilo, wakati huo, maana yake na jinsi ingekuwa.

Lakini ulimwengu mkuu wa ekumeni ulikuwa na—na mkutano na Rumi; ndipo Rumi, ambayo ni mama wa madhehebu yote. Papa, kwa mara ya kwanza katika historia, aliondoka Vatican na akaenda Yerusalemu na mahali pengi. Sasa, Yerusalemu ni makao ya kale ya dini yetu yote, ni Yerusalemu. Na katika haya makao ya kale, yule papa kutoka Rumi, ambayo imekuwa ni adui mkuu kabisa wa Kanisa nyakati zote, anaondoka anakuja kutembelea Rumi…au kutoka Rumi kwenda Palestina, Yerusalemu.

21 Na kama tunavyoona, nikiwa sina elimu, mimi mwenyewe, bila kujua ma—maneno na jinsi ya kuyanena, daima nimefundisha kwa mifano, katika mifano ya maumbile. Maumbile yatafuata maumbile. Maumbile ni ya Mungu.

Unapochukua wakati ng'ombe, wakiwa kondeni, wote wanapokusanyika pamoja pembeni mwa konde, toa ugwe wako wa kuvulia kutoka majini; samaki hawatauma. Kamwe hutawanasa hao; mnaona, ng'ombe wanapumzika; isipokuwa iwe kwamba umeutupa mahali wote wamelala. Lakini wakati ng'ombe wanapoanza kula, angalia. Mara ng'ombe wanapofanya hivyo, ndege pia watakwenda kwenye miti; wataacha kula. Mnaona, ni maumbile. Yote yanachanganyikana. Tazama nyuki, wakati huo, wanavuma juu ya asali yao, si kuikusanya. Maumbile yote hutenda kazi pamoja.

22 Na kwa hiyo, kama tunavyoona mti ukipukutisha jani, hivi karibuni sasa, katika miezi michache ijayo,

jani hilo litauacha mti. Na u—uhai, utomvu, utashuka kuingia kwenye mzizi. Na jani la mti litapukutika na kuanguka ardhini na litaoza. Na chokaa na—na chumvi-chumvi, na iko katika jani la mti, litaoza katika ardhi. Na ni jambo gani lililotukia? Uhai uliendelea mbele yake, na utalinyonya moja kwa moja ndani yake, na kulirudisha hilo jani tena. Ni mauti, kuzikwa, na kufufuka.

23 Na maumbile yote! Na mwezi ni—ni mke wa jua. Ni ile nuru ndogo. Na halafu, pia, ya kwamba wakati jua linapoondoka, katika kutokuwepo kwa jua, mwezi huakisi nuru duniani, ambayo ni mfano wa kanisa. Na wakati papa anaondoka, yule adui wa kale wa kanisa, na anakuja huku Yerusalemu, ambayoo ni makao ya kanisa; ambapo, Yerusalemu mpya na Yerusalemu ya kale; tunaona, kabla ya kutenda hilo, kulikuwa na kupatwa kabisa kwa mwezi.

24 Na katika magazeti, kote nchini kama tulivyo nayo kwenye ubao, ilionyesha jinsi mwezi huo ulivyogeuka kutoka nuru ukaingia gizani. Na matukio yake hasa, ya kwamba mwezi huo ulichorwa hasa, angani, jambo lile lile Roho Mtakatifu alilonifanya kuchora hapa miaka miwili iliyopita, na kuonyesha ninii … kufunika … Wakati ulifanyika picha sita, nilitia ile ya saba pale, kwa sababu ule wakati wa saba wa kanisa, kivuli tu cha Nuru, kwenda kwa ule… Hapo ndipo Yesu, pale mlangoni, akibisha. Lakini huo unaingia katika giza tupu.

25 Na ni taswira ya jinsi gani, ni Ujumbe wa jinsi gani kutoka kwa Mungu Mwenyewe, ya kwamba mambo haya ni Kweli! Nilishuhudia jambo hilo kwanza katika Neno Lake, kisha kwa Roho jukwaani, kisha nikalitangaza mbinguni. Hakuna kosa juu yake hata kidogo. Hiyo Mihuri na Nyakati ziko sawasawa kabisa, kikamilifu, Mungu akishuhudia kwa ishara na maajabu ya kimbinguni, pamoja na Neno na historia, yote yamewekwa pamoja, katika wakati tunaoishi sasa.

Sasa ni vigumu kwa makanisa kuona jambo hili. Ni vigumu kwa madhehebu kuliona. Wao daima wanajaribu kuwazia ya kwamba unajaribu kuwakemea watu. Hufanyi hivyo; unajaribu kuwaonya watu. Si kujaribu kuwa mwovu kwao; unajaribu kuwatoa kwenye uovu. Siyo watu waliomo katika madhehebu; ni utaratibu ambao wamo ndani yake, ndio unaowaletea laana. Watu waaminifu, wanyofu ni Wakatoliki, Waprotestanti, Wayahudi, na kadhalika. Ni wanadamu ambao—ambao …

26 Watawa hawaingii kwenye makao ya watawa kuwa wanawake wabaya; wanaingia mle kuwa wanawake wazuri. Wanajaribu kumkaribia Mungu, bali mfumo ndio unaowachafua. Watu wanajiunga na kanisa, si kuwa mtu mbaya, bali kuwa mtu mzuri. Bali mfumo wa kanisa ndio unaowatoa kwenye Neno na kanuni ambazo Mungu ameweka kwa ajili ya siku hii; na hilo ndilo linalowatoa.

27 Sasa kumbuka, Mungu ni Neno, na kila wakati Yeye ameligawa Neno kwa ajili ya kila wakati ambao ungekuwa duniani. Yeye aliligawa katika wakati wa kanisa, na ile Mihuri Saba ilifunua kila sehemu Yake. Mnaona?

Kwa nini kulikuwa na … kulikuwa na siri zilizokuwa bado zimefichwa? Ufunuo 10, tunaona, mwishoni mwa Ujumbe wa malaika wa saba, ya kwamba, siri hizi zilizokuwa zimefichwa zingefunuliwa, Ufunuo 10:1 hadi 7. Angalia, sababu ni kwamba hakukuwako na manabii katika wakati huu. Biblia ilisema, ya kwamba, "Mungu hatendi neno mpaka awafunulie manabii Wake, watumishi Wake, manabii." Na Neno la Bwana katika nyakati zote daima limewajia manabii, kamwe si kwa mfumo fulani, si kwa kundi.

28 Kamwe Mungu hakutumia kundi. Kila wakati kundi lolote la watu lilipounda madhehebu, Mungu aliliacha na kamwe hakurudi. Chunguza historia uone kama hiyo ni kweli ama si kweli. Tayari tumefanya jambo hilo. Kamwe Yeye hashughuliki na mfumo ama kundi, baada ya wao kuunda madhehebu; ni kinyume cha Mungu.

Kwa hiyo, wakati wa yale matengenezo, walikuja watengenezaji, kama vile ile Mihuri Saba ilivyothibitisha kwamba ndivyo ilivyokuwa. Lakini katika siku za mwisho sasa, ilipaswa kufunuliwa tena. Kwa sababu, tunaona katika Maandiko, katika Malaki 4, ya kwamba kutakuwa na upako utakaoshuka na kuirudisha tena ile Imani ya asili, "na kuirudisha imani ya watu kwenye pentekoste ya asili, Imani ya baba zao."

29 Nasi tulimchukua yule Eliya wa mara ya kwanza; tulimchukua Elisha kumfuata huyo; tulimchukua Yohana Mbatizaji baada ya hapo, ambaye alikuwa Elisha wa siku hiyo; na ahadi ya mwingine katika siku hii.

Sasa, Yohana Mbatizaji hakuwa Elisha wa Malaki 4. Yeye alikuwa Elisha wa Malaki 3. Yesu alisema hivyo. "Tazama, namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia." Tunamwona akiwa hivyo.

Sasa, katika kufanya hivyo, katika kupata nafasi hizo, tunajua ya kwamba Maandiko mengine yote, yaliyovuviwa na Mungu, yanatufunulia ya kwamba tuko katika siku ya mwisho.

30 Sasa, kama nikija na ujumbe wa Pentekoste, ningekuwa katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, na isingekuwa sahihi.

Hiyo ndiyo sababu Wesley asingeweza kuuchukua ujumbe wa Luther. Luther alikuwa katika wakati mmoja, wakati wa kanisa, na Wesley alikuwa katika wakati mwingine wa kanisa. Kama Yesu angalikuja katika ninii … akiwa na ujumbe wa Musa, haungetenda kazi. Kama Musa angalikuja na ujumbe wa Nuhu, haungetenda kazi.

Lakini Mungu amewagawia watu Wake—Wake—Wake, wa kila wakati, Maandiko. Na kabla ya wakati huo haujaweza kutokea, muda wake, basi makanisa yamechanganyikiwa sana hivi kwamba wao—wao hawajui waliko.

31 Hiyo ndiyo sababu wanashindwa kumtambua Yesu kuwa Mwana wa Mungu. Wao, mapokeo yao yalikuwa yameyapofusha macho yao, bali Yeye alikuwa sawa kabisa na Maandiko.

Manabii walikuwa vile vile. Yesu alisema, "Ni yupi kati yenu, kati ya baba zenu, hakuwapiga mawe hao manabii ambao walitumwa kwenu?" Ndipo Mungu anamtuma nabii Wake, kwa … na nabii ni Neno lililo hai la Mungu, likidhihirishwa.

Yesu alisema, "Mnawezaje kunihukumu Mimi, kusema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu,' nanyi mnaita, katika sheria zenu wenyewe … Ulisema, wale ambao Neno la Bwana liliwajia," ambao walikuwa ni manabii,"mliwaita 'miungu.' Nao ndivyo walivyo, kwa maana Maandiko hayawezi kuvunjwa,"Yeye alisema. "Basi mtanihukumuje?" Ambapo Yeye ni … Walikuwa sehemu ya torati, walikuwa sehemu ya Neno la Mungu, bali Yesu alikuwa utimilifu wa Neno la Mungu. Mpango Wake wote wa ukombozi, utoshelevu wote wa Mungu, ulikuwa ndani Yake.

32 Na sasa, katika nyakati za kanisa, wamefanya vivyo hivyo. Na zile Muhuri Saba zitafunua siri zote ambazo ziliachwa katika kipindi hicho, kwa sababu hatukuwa na manabii, na Neno haliwajilii watengenezaji. Manabii!

Mungu habadiliki. Katika Malaki 3, ilisema, "Mimi ni Mungu, wala sibadiliki." Njia ya kwanza ya Mungu kutenda jambo lo lote, hiyo ndiyo njia ya Mungu ya kutenda lo lote. Mungu aliamua angemwokoa mwanadamu kwa Damu iliyomwagika ya Mtu asiye na hatia, katika bustani ya Edeni, Naye hajaibadilisha tangu wakati huo, na hawezi kuibadilisha. Tumejaribu, kwa elimu, kwa majumba, kwa taratibu, kwa madhehebu, kwa maadili, na cho chote kile, na zote zimeshindwa. Lakini kuna mahali pamoja tu ambapo Mungu hukutana na mwanadamu, hiyo ni, chini ya Damu iliyomwagika ya asiye na hatia. Ni kwa Damu tu! Huo ulikuwa ndio uamuzi Wake wa kwanza. Mnaona?

Tunaweza kufanya uamuzi, na mwaka ujao tunaweza kuwaza vizuri zaidi. Tuna wazo bora zaidi juu yake, mwaka ujao. Mungu hawezi; Yeye hana kikomo. Uamuzi Wake wa kwanza ni mkamilifu; hakuna jambo linaloweza kuuondoa. Ninaweza kujifunza zaidi; sisi tuna kikomo. Ninaweza kujifunza zaidi; unaweza kujifunza zaidi. Lakini Mungu hawezi kujifunza zaidi; Yeye ni mkamilifu, kwanza. Na, kwa hiyo, uamuzi Wake wa kwanza, iweke nafsi yako juu yake. Kile Biblia isemacho, hivyo ndivyo ilivyo!

33 Mungu hana budi kuuhukumu ulimwengu siku moja. Na Mkatoliki anasema Yeye atauhukumu kwa kanisa Katoliki. Kama hiyo ni kweli, ni kanisa Katoliki lipi? Wanatofautiana, mmoja kwa mwingine. Kama ukienda kuhukumu kwa Kiprotestanti, ni kanisa gani la Kiprotestanti? Wanatofautiana, mmoja kwa mwingine. Na ingekuwa ni kutatanisha kidogo; hakuna mtu angejua mahali pa kusimama. Kama Mmethodisti yuko sahihi, Mbatisti amepotea. Kama Mprotestanti yuko sahihi, Mkatoliki amepotea; Mkatoliki ni sahihi, Mprotestanti amepotea.

Lakini Biblia ilisema ya kwamba Yeye atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo, Naye ni Neno. Ndipo, Yeye atauhukumu kwa Neno.

Na madhehebu yote yanaondoka kwenye Neno hilo, kutengeneza kanuni zao za imani. Ninaomba tu ye yote anithibitishie ambapo wanalichukua Neno kamili. Hawawezi kufanya jambo hilo, kwa sababu linatawaliwa na mfumo wa mwanadamu. Ambapo una mtu …

Mungu kamwe hakushughulika ila na mtu mmoja kwa wakati mmoja. Hata hakuwa na manabii wawili kwa wakati mmoja. Mmoja! Mungu anaweza kumshika mtu mmoja mkononi Mwake. Yeye hawashughulikii … madhehebu yenu; Yeye hushughulika na wewe.

34 Sasa, juu ya msingi huo, tunakuja kwenye sikukuu ya baragumu, zile siri zilizofichwa. Imetabiriwa ilikuwa iwe hivyo, kwa hiyo ilibidi ifunuliwe jinsi ilivyokuwa. Lakini kufunuliwa katika siku hii ya mwisho, kutimiza hasa yale niliyosema hivi punde, Malaki sura ya 4, Luka sura ya 17 na—aya ya 30, jinsi Yeye angefanya jambo hilo, na Waebrania 13:8, Waebrania 4:12, na mengi ya hayo Maandiko yanayotuambia. Sasa, kama hilo ni geni kwa baadhi yenu, hebu niseme ya kwamba Mungu daima … Jinsi Mungu anavyojulikana miongoni mwa watu ni kwa kuwa kinabii.

Wayahudi daima walijua kuwaamini manabii wao. Yeye alisema, "Kama kuna mmoja miongoni mwenu, Mimi Bwana nitazungumza naye katika ndoto za kiroho na katika maono. Na, yale anayosema yanatimia, basi msikieni." Wao daima walikuwa …

Hivyo ndivyo walivyoshindwa kumtambua Yesu, na iliwabidi kumfanya kitu kingine, kwa hiyo wakamfanya pepo mchafu, "Beelzebuli," kwa sababu Yeye aliweza kutambua mawazo yaliyokuwa mioyoni mwao. Daima tunajua ya kwamba hiyo ni ishara ya Neno.

35 Waebrania sura ya 4, aya ya 12, kasema, "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

Yeye atawakumbusha mambo haya ambayo nimewaambia, na atawaonyesha mambo yajayo."

"Mungu katika nyakati mbalimbali, kwa njia nyingi," Waebrania 1, "alisema na baba zetu katika manabii, katika hizi siku za mwisho amesema nasi katika Mwana Wake, Yesu Kristo." Mungu yeye yule, alibadilika tu kutoka kwa manabii hadi kuwa Mwana. Hivyo tu. Mnaona? Daima Ujumbe ule ule, njia ile ile ya kufanya jambo hilo.

36 Sasa, imetabiriwa ya kwamba makanisa yangekuwa katika hali hii, yalipaswa kurejeshwa upya tena. Naye alisema, katika Malaki 4, ya kwamba Yeye "angemtuma Eliya nabii, na angewarudisha wa—watu warudi tena," pamoja na … kuileta. Angalia. Na kabla tu … Ama, mara baada ya Ujumbe wake, kutakuwa na wakati ambapo ulimwengu utawaka moto, na wenye haki watatembea juu ya majivu.

Sasa, kwa mwanatheolojia fulani ambaye huenda anasikiliza kwenye kanda, mahali fulani kote ulimwenguni, kama unafikiri kwamba huyo alikuwa ni Yohana, kumbuka, basi, yale Maandiko yamekosea, kwa kuwa ulimwengu haukuwaka baada ya ujumbe wa Yohana. Yesu hakuja na kuwachukua watu katika ule Utawala wa Miaka Elfu; bali Yeye ameahidi kufanya jambo hilo baada ya Roho wa Eliya kuja duniani tena.

37 Angalia sasa katika Malaki 4, tunaona hapa ya kwamba jambo hili linapaswa kufanywa kurudisha (nini?) Imani ya watu kurudi kwa baba wa asili, Fundisho la pentekoste, wale baba wa asili. Naye atawarudisha watu kwa baba zao.

Tunaona katika Luka 17, Yesu alisema ya kwamba wakati alipokuja katika siku hizi za mwisho, Luka 17:33, tunaona ya kwamba Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Mwanadamu, wakati Mwana wa Adamu anapofunuliwa."

Sasa angalia, Yeye alikuja katika majina matatu ya wana. Yeye alikuja katika jina la Mwana wa Daudi … Ama, Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi.

38 Sasa, ilimbidi Yeye kuja kama Mwana wa Adamu, kwa sababu Yeye alikuwa ni Nabii. Yehova, Mwenyewe, aliwaita manabii, "mwana wa Adamu." Na Yesu kamwe hakujiita Mwenyewe kama Mwana wa Mungu. Yeye alijiita Mwenyewe, daima, kama Mwana wa Adamu. Na angalia, Yeye alijifunua wakati huo kama Nabii, Mwonaji. Kasema, "Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiziamini." Yeye alitimiza kila sifa iliyonenwa juu Yake katika Maandiko, hata kwenye kifo Chake, kuzikwa, kufufuka; Kusulubishwa Kwake, kuzaliwa Kwake, yote. Na katika kazi Yake, Yeye alitimiza sifa za Mwonaji, Mwana wa Adamu.

39 Sasa Yeye amekwisha kufunuliwa kupitia nyakati za kanisa, sasa angalia, kupitia nyakati za kanisa, kama Mwana wa Mungu. Mungu akiwa Roho, Roho Mtakatifu, Yeye alijifunua katika nyakati za kanisa kama, katika kusanyiko, kama Roho Mtakatifu miongoni mwa watu.

Tunaona, katika Wakati wa Kanisa la Laodikia, ule wakati wa mwisho wa kanisa, Yeye anatolewa nje ya kanisa. Hakuna mahali pengine ambapo Yeye aliwahi kufukuzwa, katika wakati wo wote, ila katika Wakati wa Laodikia. "Kwa sababu, wao walisema, 'Sisi ni matajiri wala hatuhitaji cho chote.' Wala hujui ya kwamba wewe ni mwenye mashaka, maskini, uchi, na kipofu, wala hujui." Alifukuzwa katika wakati wa kanisa.

Halafu basi, kulingana na Luka 17, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Sasa, Yeye alikuwa akisoma Mwanzo ule ule tunaousoma. Angalia, huko Sodoma, kile kilichotukia. Ilikuwaje Sodoma? Ibrahimu …

40 Daima kuna tabaka tatu za watu. Kulikuwako na Ibrahimu, mteule na aliyeitwa atoke, nje ya Sodoma yenyewe. Kulikuweko na Lutu, mfuasi wa kanisa, ama mtu wa kimadhehebu, kule chini; alikuwa amekuwa sehemu ya ulimwengu huo, kwa kuwa meya wa lile jiji, alikaa kwenye lango; alikuwa hakimu, ambaye ni meya. Na kulikuwa na Sodoma, yenyewe.

Sasa, wakati wa jioni, ama mchana, wakati Ibrahimu alipokuwa chini ya mwaloni wake, Malaika watatu wakamtokea. Wawili wao walishuka wakaenda Sodoma, na kuihubiri Injili na kujaribu kuwaita watoke. Wasingefanya hivyo; walikuwa wamepotoshwa. Lutu, na mkewe, tu, na binti zake wawili, walianza kuondoka. Na mkewe akageuka nyuma akawa nguzo ya chumvi.

41 Lakini Yule aliyekaa na kuzungumza na Ibrahimu, ambaye Ibrahimu alimwita, "Elohimu, Mwenyezi." Mwanzo 1, "Mungu! Hapo mwanzo, Mungu,"Elohimu, Yeye—Yeye ajitoshelezaye kwa yote, Yeye anayeishi kwa nafsi Yake. Ibrahimu alimwita, "Elohimu." Ndipo akaketi na kula pamoja na Ibrahimu; Akanywa; Yeye

alikuwa katika mwili wa kibinadamu. Na angalia ishara aliyompa Ibrahimu.

Sasa, walikuwa wakimtazamia mwana anayekuja, mwana aliyeahidiwa, Isaka. Miaka ishirini na mitano, katika safari ndefu, walikuwa wamemtazamia, bali walikuwa mwisho wa safari. Mungu alikuwa ametokea katika namna nyingi, kama alivyofanya katika nyakati za kanisa, katika Nuru, na kadhalika, kama alivyonena na Ibrahimu, na kwa sauti. Lakini kabla tu ya kuja kwa mwana … Sasa tumepitia hayo, nanyi mnajua ninayarudia tu, kuwaeleza jambo hili. Kwamba, Yeye aliubadilisha mwili wa Ibrahimu na Sara, mara baada ya jambo hili, kusudi wapate kumpokea mwana.

Angalia, ishara ya mwisho waliyoipata, kabla mwana huyo hajaja, ilikuwa ni Yehova akinena nao katika umbo la mwanadamu. Na jinsi walivyojua huyu alikuwa ni Yehova, kwa sababu Yeye alisema, "Ibrahimu," si Abramu. Siku chache tu kabla, Mungu alikuwa amebadilisha jina lake. "Yu wapi mkeo, Sara?" Si S-a-r-a-i; lakini S-a-r-a, "binti mfalme."

Naye Ibrahimu akasema, "Yumo hemani, nyuma Yako."

Naye akasema, "Mimi," hicho ni kijina nafsi, "Nitawazuru kulingana na ahadi Yangu. Wakati wa maisha, siku ishirini na nane zijazo, jambo fulani litatukia kwa Sara."

Naye Sara, kwenye hema, akatabasamu kindani, akasema moyoni mwake, "Jambo hili linawezekanaje, niwapo mkongwe; nipate furaha na bwana wangu, ambaye pia ni mzee, Ibrahimu?"

Kisha yule Malaika, ama yule Mtu, akasema, "Mbona Sara akasema hivyo moyoni mwake?" Katika hema nyuma Yake! "Kwa nini alisema mambo haya hayawezekani?" Mnaona? Mtu katika mwili wa kibinadamu, kama nabii, hata hivyo ilikuwa ni Elohimu akitambua wazo lililokuwa moyoni mwa Sara, nyuma Yake.

42 Naye Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika ukamilifu wa dahari, wakati Mwana wa Adamu," si Mwana wa Mungu, "wakati Mwana wa Adamu atakapokuwa akifunua."

Hatukuwa na jambo hilo kote katika wakati. Mnaona mwendelezo huo mkamilifu wa Maandiko? Hapa tunaishi ndani yake. Zile siri; hata ya ubatizo katika Jina la Bwana Yesu, na mbali na wazo la Umoja; na mambo haya mengine, jinsi Roho Mtakatifu ameliingiza hilo ndani na kulionyesha kikamilifu; na ule Ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu, ile Ishara, na kila kitu, na akakiweka; na jinsi alivyomweka kila mtengenezaji na kila kitu, sawasawa kabisa. Na, mnaona, moja kwa moja mbele ya macho yetu wenyewe, na haiko pembeni. Inajulikana ulimwenguni. Yesu, Mwana wa Mungu, akijifunua Mwenyewe kwa Maandiko, akilifanya Andiko hilo ambalo limechaguliwa tangu zamani kwa ajili ya siku hii, kama ilivyokuwa katika siku ile na siku zingine zote, liishi. Na, kuamini Hilo, ndio dhihirisho la Roho Mtakatifu.

43 Haki, huwezi kutamka ya kwamba "kwenda kanisani" tu ni ushahidi wa Roho Mtakatifu. Kama ukifanya hivyo, basi hao Mafarisayo walikuwa Naye. Mnaona? Huwezi kutamka "kutetemeka au kuruka" kuwa … Kama ukifanya hivyo, makafiri wanaye. Kama ukisema "kunena kwa lugha," ni—ni ibada gani ya ibilisi isiyonena kwa lugha? Niambie moja.

Ndugu Jackson anayeketi hapa kwa ajili ya Afrika, kutoka Afrika, angeweza kukwambia jambo hilo. Nimekuwa kwenye kambi za Wahindi huku, nikaona wachawi na walozi wakijijikatakata, na kumwaga damu yao wenyewe, na kunena kwa lugha; na—na mchawi anafasiri hayo, na nikawaona wakiweka penseli chini na kuandika katika lugha zisizojulikana. Kwa hiyo hilo silo. Lakini kama …

Ushahidi wa kweli ni nini? Yesu alisema, "Kwamba mnaamini ya kwamba Mimi Ndiye." Naye ni Neno.

44 Kwa nini hawakulipata? Kwa nini Wayahudi hawakulipata? Wao walikuwa watu wenye haki; walikuwa watu wema; walikuwa watu watakatifu, na kulikuwa na watu wa kila namna; lakini, kwa wale waliochaguliwa tangu zamani kulisikia Neno!

"Na unajuaje kama ni Neno? Kila mmoja anasema hivi."

Ni ahadi ya Biblia ikithibitishwa ya wakati huo, basi, basi unarudi mahali alipo Roho Mtakatifu. Angalia sauti ya Baragumu katika dakika chache, kile inachotangaza. Ile Baragumu, Baragumu ya Injili, angalia ni nani anayeweza kuisikia. Kumbukeni, wale walio katika miji yenye kuta hawangeweza kutoka katika yubile. La, bwana. Walikuwa kwenye kuta; walikaa pale. Ilikuwa imekwisha; walikuwa watumwa maishani mwao mwote, na ilibidi watiwe alama. Sasa tunapoona mifumo hii yote, angalia.

45 Sasa, matendo haya, Malaki 4, na haya yote, na Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele," Yeye hudumu milele ni Neno, Neno lililodhihirishwa. Hivyo ndivyo hasa alivyowatangaza manabii. *Nabii* halimaanishi tu "mwonaji ama mtabiri;" linamaanisha "mfunuzi wa Neno lililoandikwa." Katika maisha yake mwenyewe, kazi zake mwenyewe, hufunua na kuthibitisha Neno la siku hiyo; kama vile Nuhu alivyojenga safina; Musa kule chini; cho chote kile; na ahadi yoyote, Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati huo.

46 Sasa tunajua ya kwamba Yeye yuko pamoja nasi. Tunaamini jambo hilo. Mnaona Neno Lake likidhihirishwa, kwa picha, kwa Maandiko, kwa matamshi Mbinguni, duniani, kila kitu kingine alichosema. Hakuna hata wakati mmoja liliwahi kushindwa. Ninamwomba mtu yeyote anionyeshe, kutoka sehemu mbalimbali nchini, ama kote ulimwenguni, una—unawajibika kuniandikia na kuniambia, ambapo wakati mmoja liliwahi kushindwa. Kamilifu, neno kwa neno, sasa, hiyo ni ahadi.

47 Kwa nini alipaswa kuonekana katika siku hizi za mwisho? Kama ukirudi nyuma, na ninyi wasikilizaji wa kanda, kwenye *Mti wa Bibi-arusi*, na kuleta mahali Kristo alipokuwa, ule Mti uliokuwa katika bustani ya Edeni. Adamu wa kwanza aliyeanguka; na huyu Adamu wa Pili alikatiliwa mbali na dhambi. Wao walimsulubisha kwenye mti wa Kirumi, na kutoka humo ukatolewa…ukatoka Mti wa Bibi-Arusi ambao aliahidi, ambao tunauona katika Maandiko, sasa, kusudi ampate Bibi-arusi.

Kama vile piramidi, jinsi ilivyokuja katika uchache wakati wote, kutoka kwenye ule upana mkuu; kutoka kwa Luther, Wesley, Pentekoste, halafu jiwe la kufunika kwenye kilele chake limechongoka hivyo, na kila moja ya mawe hayo yamewekwa pamoja kikamilifu sana. Nasi hatujui bado jinsi walivyofanya jambo hilo, bali limewekwa kikamilifu kabisa katika piramidi hiyo! Nasi si mafundisho ya piramidi sasa, tunaninii tu …

Henoko na hao wengine waliijenga, miaka mingi iliyopita, nayo inasimama kama mfano. Kama tu vile jua linavyochomoza na kutua; kama vile tu mti hupukutisha lake, jani lake, na kuchipuka tena; kama samaki, na ng'ombe, na kila kitu kinavyoonyesha mfano wake. Hiyo piramidi inasimama kama mfano.

48 Nenda kwenye chumba cha nabii na uangalie hizo hatua saba. Ni wapi—ni wapi mlinzi alipopata changamoto ya kumleta yule anayekuja mbele ya mfalme? Juu ya vipandio; alikuwa katika hatua ya saba. Hapo inaonyesha ya kwamba hatuna budi kuja tena na Roho yule yule aliyekuwa juu ya Yohana; alimtambulisha Masihi. Yeye alikuwa mkuu kuliko manabii wote; alilianzisha. Nasi hatuna budi kufikia mahali, tena, kwenye kitu fulani kitakachomtambulisha Masihi.

49 Na Masihi ataninino vipi…watu wanaomwamini watajua jambo hilo vipi isipokuwa wawe daima katika Neno, kujua Yeye ni nani! Danieli alisema, "Wenye hekima watajua; bali wajinga, wasio na hekima, wasingejua. Watamjua Mungu wao." Sasa, sasa, jinsi atakavyoonekana katika siku za mwisho, ni kuwarudisha watu kwenye Neno, ili kwamba Bibi-arusi atamjua Mumewe, amjue Mwenziwe, Neno lililofunuliwa. Hiyo ndiyo sababu jambo hili halina budi kutukia.

Haikuwa katika wale watengenezaji; haikuwa katika Luther, Wesley, na—na Wapentekoste, na hao wengine. Maandiko yanasema haikuwa hivyo.

Lakini itakuja. Hiyo ndiyo ahadi Yake kwa ajili ya wakati huu. Tunaishi katika wakati ambao Kuja Kwake kutakuwako. Bibi-arusi hana budi kutambulishwa ndani Yake. Mwanamke yeyote hana budi kutambulishwa na mumewe, kwa kuwa hao wawili ni mmoja. Na Bibi-arusi wa Kristo hana budi kutambulishwa pamoja Naye, kwa kuwa hao wawili ni Mmoja; Naye ni Neno, si madhehebu. Neno! Tunapaswa kuwa watoto wa Nuru, na Nuru ni Neno lililofanywa Nuru kwa ajili ya wakati huu. Tunajuaje Nuru isipokuwa itoke kwa Neno? Vema. Neno lililofanyika mwili ndilo Nuru ya ulimwengu; unapoiona, na Biblia ilisema hivyo.

50 Hao watu wakimwangalia Yesu pale, na kusema, "Vema, Mtu huyu, Yeye ni nani? Mbona, Yeye amezaliwa, kuzaliwa haramu kule chini. Mbona, baba Yake na mama yake ni *hivi*, *vile*, na *vinginevyo*, na haya yote pale." Lakini hawakumjua. Kama wangeyajua Maandiko, wangalimjua Yeye. Yeye alisema hivyo.

Wakasema, "Sisi ni wanafunzi wa Musa!"

Kasema, "Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi, kwa kuwa Musa aliandika habari Zangu." Na bado ni vipofu sana kuweza kuliona!

Mnaona jinsi walivyo wanyenyekevu? Mbali na wahudumu wote, na madhehebu, na kanuni za imani, na kila kitu. Mungu aliingia moja kwa moja ndani, katika mwili, katika umbo la Mwanadamu, Mkombozi aliye Jamaa wa Karibu.

Hana budi kutambulishwa pamoja Naye. Tumealikwa kuwa watoto wa Nuru, tupate kutembea katika Nuru.

51 Ninakumbuka huko chini Kentucky, hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa na mkutano. Kule nje, baada ya mimi kutoka kanisani, kulikuwa na mzee mmoja amesimama, akiwa na taa mkononi mwake. Yeye alikuwa mfuasi wa kanisa ambalo haliamini katika uponyaji, na kadhalika. Kasema, "Mimi—mimi ninapingana nawe, Ndugu Branham."

Nikasema, "Vema, una haki ya kufanya hivyo."

Yeye alisema, "Unaona, sitakubali chochote isipokuwa nione. Sina budi kuliona, dhahiri kabisa."

Nikasema, "Basi je! Ulipata kumwona Mungu, dhahiri kabisa, akisimama mbele yako?" Bila shaka, yeye hakuamini katika maono na kadhalika.

Akasema, "La."

"Mbona," nikasema, "basi wewe si mwamini, bwana. Nisingeweza kuzungumza na wewe. Mnaona? Mnaona? Tunaona kile Mungu anachoahidi na kushikilia Hicho."

Akasema, "Unaonaje hilo?" Nikasema … Akasema, "Njoo, twende nyumbani pamoja nami tuzungumze usiku wa leo."

Nikasema, "Siwezi; ningetaka kufanya hivyo. Unaishi wapi?"

Akasema, "Unapanda mlima huu hapa."

Nikasema, "Utafikaje kule? Huioni nyumba yako." A-ha. A-ha. Naam. Naam.

Akasema, "Vema, kuna njia inayoenda juu ya kilima."

Nikasema, "Huioni njia." A-ha.

Akasema, "Vema, nina taa."

Nikasema, "Hiyo taa haitatoa mwangaza wa kufika moja kwa moja nyumbani mwako. Loo, la. Lakini njia hiyo itaongoza hadi kwenye nyumba. Lakini taa hiyo itaonyesha tu nuru kwa hatua moja kwa wakati."

52 Tutatembea katika Nuru, ile Nuru nzuri; hatua moja kwa moja, Bwana, ukimkaribia Yeye. Naam. Enyi watoto wa Nuru, likubalini Neno Lake, endeleeni kutembea kisha mwangalie hayo mengine yakijifunua. Usiliache, haidhuru mtu mwingine anasema nini. Dumu moja kwa moja katika Hilo na uendelee tu kutembea Nalo, ulitazame likijieleza na kujifunua Lenyewe. Neno ni Mbegu; mbegu katika udongo unaofaa itazaa aina yake.

53 Angalia Ufunuo 10:1 hadi 7, siri zote zinapaswa kufunuliwa kwa Bibi-arusi, na mjumbe wa Kanisa la Laodikia. Kuna mtu ye yote aliye na Biblia ya Tafsiri Ilirudiwa? Kama unayo, utaona kwamba mahali pale iliposema, "malaika," limetengwa katika mabano na linasema, "yule tai." Mnaona? A-ha. A-ha. Mnaona? Yule mjumbe kwa—kwa Kanisa la Laodikia, mnaona, Ufunuo 10:1 hadi 7.

Naye alisema ya kwamba hii … katika siku ile alipomwona akishuka, naye akakila kile kitabu kidogo. Na kulikuwa na … "Aliweka mguu mmoja juu ya nchi kavu, na mmoja juu ya bahari, na akaapa kwa Yeye aishiye, milele na milele, ya kwamba, 'Wakati hautakuwapo tena.'" Na wakati alipofanya hivyo, Ngurumo Saba zikatoa sauti zao. Na wakati zile Ngurumo Saba zilipotoa sauti zao, Yohana alisema alikuwa karibu kuandika. Naye akasema, "Usiyaandike." A-ha. Mnaona? Naye akayatia muhuri.

54 Sasa, mtu fulani alisema, "Vema, hiyo Mihuri Saba, basi, Ndugu Branham, hiyo itafunuliwa katika siku za mwisho, siri fulani kuu jinsi tunavyomkaribia Mungu?" La, bwana, haiwezekani.

"Ye yote atakayeondoa Neno moja kutoka kwenye Biblia hii, ama kuongeza neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa, Kitabu cha Uzima." Hayo ni nini, ni ufunuo juu ya yale yaliyoachwa huko nyuma, kuyaleta. Tayari imeandikwa Hapa. Limo humu ndani. Ni kufunua yale ambayo tayari yameandikwa. Mnaona? Maana, huwezi kuongeza jambo moja Kwake, ama kuondoa Neno moja Kwake.

55 Sura ya kwanza ya Ufu- … ya—ya Biblia, hapo mwanzo, Mwanzo. Mwanamke mmoja hakuliamini Hilo, bali alilifasiri tu vibaya, akamwacha Shetani amfasirie vibaya, neno moja, "hakika." Mnaona? Halafu basi, kutokana na hilo, ilisababisha shida hii yote. Na huyo alikuwa ni Mungu akinena, Neno la Mungu.

Na katika mlango wa mwisho wa Ufunuo, Yesu Mwenyewe, Mungu yeye yule, alisema, "Ye yote atakayeondoa Neno moja, ama kuongeza neno moja Kwake."

Huu ndio ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo. [Ndugu Branham anapigapiga Biblia yake — Mh.] Na zile Muhuri Saba zilikuwa zimeficha zile siri, ya zote zilikuwa nini; na zinapaswa kufunguliwa katika siku ya mwisho, kwenye wakati wa Laodikia, mwisho wa wakati. Mungu ashukuriwe! Hilo linamalizia Ujumbe kwa Kanisa. Hilo linaumaliza. Wanapoangalia nyuma na kuona jinsi mambo yamekuwa, na kuona mahali yote yamefikia, hilo linaumalizia, wakati wa Kanisa.

56 Sasa angalia baragumu tunazozungumzia, ni kuitwa pamoja aidha kwa ajili ya sikukuu, kwa ajili ya vita, kwa ajili ya mtu fulani, siku fulani takatifu, ama kitu kama hicho. Angalia. Unasema, "Kwa ajili ya mtu fulani?" Naam. Ama, kwa ajili ya mwaka wa yubile, kutangazwa kwa kuja kwa uhuru, wakati wangeweza kurudi; sasa, tungeweza kuchukua asubuhi kamili juu ya jambo hilo moja tu. Lakini, sasa, kuingia kwenye zile baragumu. Una msingi sasa, wa ile Mihuri na Kanisa, sasa tunaingia kwenye baragumu. Baragumu ililia, na baragumu inaashiria ama vita, ama siku ya sikukuu. Ama, maana yake, ni,

"kukusanyika pamoja kwa watu," baragumu.

Paulo alisema, "Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani awezaye kujiandaa kwa vita, ama kwa ajili ya amani, ama cho chote kile?" Ni nani ajuaye? Unapaswa kujua maana ya mlio wa baragumu.

Kwa hiyo, wakati baragumu inapolia, tunaona kitu fulani duniani leo. Kuna shida kubwa mahali fulani. Kila mtu anajua jambo hilo. Kila mtu ameshikwa na fadhaa. Ulimwengu mzima ni ulimwengu wa fadhaa, nasi tunajua kuna kasoro fulani. Pentagon, kila mahali, tunajua kuna kasoro fulani.

57 Sasa, njia pekee utakayojulia mlio wa baragumu, ni kuangalia yale ile Karatasi ya Muziki inayosema. Mnaona? Hivyo tu. Ni taarabu kuu, mnaona, na mapigo yake.

Kama vile, *Petro na Mbwa Mwitu*, unaona, wakati wewe … kama ninii … Na yule—mtunzi ameandika kitabu, na mkurugenzi hana budi kuwa katika roho ile ile ya mtunzi. Kama hayuko hivyo, yeye anatoa mapigo mabaya, halafu jambo lote linavurugika.

Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Tuna wakurugenzi wengi mno katika … si katika Roho wa Mtungaji. Wanasema, "Madhehebu, vema, tunaamini jambo *hili*."

Haidhuru unasema nini, Biblia ni kweli. Ukiupiga kulingana na Karatasi ya Karata papa hapa mbele yake, kisha ule mpangilio wa sauti wa tendo kuu la Mungu linaucheza sawasawa kabisa, ndipo tunaweza kuiona ile saa na mahali tunaposimama.

58 Sasa angalia, baragumu ni kuwaita watu pamoja, kukusanyika pamoja kwa ajili ya jambo fulani. Wakati mwingine ilimtangaza mtu mashuhuri.

Kama vile katika Yusufu, wao waliipiga baragumu, naye Yusufu alikuwa anatokea; ambalo ni m—mfano wa "ile Tarumbeta Kubwa" tunayonena habari zake, na tutaifikia baada ya kitambo kidogo, katika Isaya. Hiyo inasema, "Wakati Baragumu Kuu itakapolia, wakati bendera hiyo itakapoinuliwa, juu kule; na ndipo utakuja wakati ambapo Baragumu Kuu itapigwa, na mataifa yote yatakusanyika Yerusalemu." Hapo ndipo ule Utawala wa Miaka Elfu utakapoanza; ile Baragumu Kuu.

59 Sasa, wito huu, wa sikukuu ya baragumu, kukaribia kwa kitu fulani. Angalia Ufunuo 8:7, kama unataka kuandika. Tunaona Baragumu ya Kwanza, kulikuwa na mvua ya mawe, damu, moto, juu ya nchi; sawasawa tu na Kutoka, wakati Mungu alipokuwa akiwaita watu Wake watoke, ya kule kutoka.

Sasa, sababu ya hizi Baragumu Saba kutokuwa na uhusiano na Kanisa hili na wakati huu, ni kwa kuwa hizo ni kwa ajili ya Israeli peke yao. Ni wito, wa kukusanyika kwa watu. Na sasa kuna umuhimu mmoja tu humu ndani ambao ninawataka mfikie, katika dakika chache, ni mahali ambapo mtaona ni kwa nini jambo hili halihusu wakati huu tunaoishi; zile Baragumu Saba.

60 Najua watu wengi hawakubaliani na jambo hilo, bali najua ndilo hili. Ninajua jambo hilo. Si kwa sababu ninasema mnasema jambo hilo; kwa sababu, sikulipata kutoka kwangu mwenyewe. Mawazo yangu—yangu si yangu mwenyewe. Cho chote kile kilichoniambia jambo hilo, kama kimekosea, basi kimekosea. Bali sisemi jambo hili kwa nafsi yangu, ninasema yale Mtu mwingine amesema. Huyo Mtu mwingine ndiye Mungu aliyenena nasi na kufanya mambo haya yote ambayo amefanya, na akajitokeza, mnaona, kwa hiyo ninajua ni kweli.

61 Kule—kule kukusanyika kwa Israeli ni Baragumu. Zile baragumu ni za kukusanyika Israeli. Angalia, ile Baragumu ya Kwanza kabisa inalia; damu, moto, mvua ya mawe, na kila kitu, vinatawanya ardhi. Mnaona? Alikuwa akifanya nini? Akiwaleta Isreli kutoka Misri ya kiroho, mnaona, kurudi katika nchi ya uenyeji wake.

Sasa hebu niseme jambo hili papa hapa, ya kwamba, kila Baragumu iliyopigwa, ilipigwa chini ya Muhuri wa Sita. Tutafikia jambo hilo katika dakika chache, mahali tulipozipata zile Muhuri pale. Baragumu zote zilipigwa chini ya Muhuri wa Sita.

Kwa sababu, ule Muhuri wa Saba, kulikuwa na kimya. "Hakuna mtu aliyejua; hiyo ilikuwa ndiyo dakika ama saa ambayo Kristo angekuja," kama alivyotufunulia sisi.

62 Lakini kila Baragumu ilipigwa chini ya Muhuri wa Sita, chini ya mateso ya Wayahudi. Angalia, Ufunuo sasa, wa 8, na uanze na kifungu cha 7. Zote zilikuwa ni kule kuitwa kwa Israeli, ya asili, kule Misri; sasa ni kuitwa kwa Israeli, kwa maana ya kiroho. Alikuwa akiwafanya wawe tayari kuja kwenye sikukuu ya Upatanisho.

Angalia, sikukuu ya baragumu ilikuwa ya kwanza, ambayo ilikuwa pentekoste. Sikukuu ya upatanisho iliifuata, siku hamsini baadaye. Sikukuu ya upatanisho, isome hapa. Tutaweza, labda, tukiwa na wakati, tutalirejea na kuwasomea kutoka katika Biblia, hapa katika Mambo ya Walawi 12, sasa, au Mambo ya Walawi 23, hasa, na Mambo ya Walawi 16. Tunaona ya kwamba kwanza ilikuwa ni sikukuu ya—ya baragumu. Ilikuwa ule upatanisho na ile…baada yake ilifuata pentekoste, sasa tunaona … Sikukuu ya

upatanisho ilifuata sikukuu ya baragumu.

63 Sasa angalia, Baragumu ilipigwa, na hiyo ilikuwa ni kuwakusanya pamoja. Sasa, Baragumu ya Kwanza ilipigwa, kulikuwa na mvua ya mawe, damu, moto, uliopuliziwa juu ya nchi, kama tu vile ilivyokuwa Misri, ikijitayarisha kuwaita kwenye Siku ya Upatanisho. Mnaona? Waliukataa Upatanisho wa kweli. Na miaka hii imeongezwa kupitia hapa, umekuwa mwaka wa pentekoste. Mnaona? Sasa sauti ya Wayahudi inafuata.

Huku kumekuwa ni kuitwa kwa Kanisa. Angalia kwa makini sana. Sasa, jambo ambalo, baadaye, Yeye aliwachukua akawapeleka kwenye nchi ya ahadi; ambapo atafanya jambo lile lile, ambalo, kwa njia ya mfano, Yeye analichukua Kanisa na kulipeleka kwenye nchi ya ahadi.

Kumbukeni, kila Baragumu ilipigwa chini ya Muhuri wa Sita, ndipo tu ilipolia.

64 Angalia sasa, hasa, mwendelezo wa Maandiko, ni sawa kabisa. Chini ya Baragumu ya Saba, kwa Israeli ni sawa na vile Muhuri wa Saba ulivyokuwa kwa Kanisa. Tunaona, chini ya Muhuri wa Saba, ya kwamba wakati watu hawa waliokuwa chini ya madhabahu pale, waliopokea mavazi … Walipewa nguo ndefu, si kwamba walizipata, kwa sababu walikuwa katika kipindi cha wakati Mungu alipokuwa angali akishughulikia neema kwa Mataifa, si Wayahudi. Israeli imeokolewa kama taifa. Mungu hushughulika na Israeli kama taifa. Mataifa ni "watu kwa ajili ya Jina Lake," si taifa kwa ajili ya Jina Lake. Israeli!

65 Na wakati Hitler na hao wengine walipowatesa Wayahudi, na kufanya mambo waliyofanya chini ya huo; angalia, wao, Stalin, Hitler, na hao madikteta wote walikuwa wameinuka. Kama tungalikuwa na wakati, ambao, kuyarudia kwa baadhi ya wageni, bali tumepitia jambo hilo. Chini ya wakati uo huo, ambapo kumekuwa na Ujerumani na—na mataifa mengine yote, Wayahudi wametawanyika katika nchi zote. Lakini kumekuwako, katika miaka ishirini iliyopita, mateso makali dhidi ya Wayahudi.

Nimekuwa huko nje mahali pa kale ambapo waliiteketeza miili yao, na kuichoma, na kutumia … walitumia majivu yao kurutubisha ardhi, watoto wa Kiyahudi, na wanawake, na kila kitu. Halafu wao wanajaribu kukana jambo hilo; wanawachukua na kuwapeleka huko nje na kuwaonyesha mahali jambo hilo lilipotendewa.

Imekuwa ni mateso makali dhidi ya Israeli, kwa sababu imekuwa wakati wa kumwita sasa arudi kwenye Upatanisho. Yeye angali chini ya upatanisho wa mwana-kondoo wa kawaida. Mwana-Kondoo halisi wa Mungu ni Upatanisho, naye ameukataa, na Damu imekuwa juu yake tangu wakati huo. Angalia, kuwaweka hao watu tayari! Jinsi ambavyo basi Baragumu ya Saba na Muhuri ya Saba ni kamilifu, kikamilifu pamoja, mateso ya Wayahudi.

66 Angalia, katika Ufunuo sura ya 9 na kifungu cha 13, sasa angalia kwa makini sana, chini ya Baragumu ya Sita. Ufunuo 9:13, chini ya Baragumu ya Sita, kumbuka, kulikuwa na wapanda farasi laki mbili ambao walikuwa wamefungwa katika mto Frati, waliachiliwa chini ya Baragumu ya Sita. Sasa hakuna wapanda farasi laki mbili ulimwenguni; bali kulikuwa na wapanda farasi laki mbili. Angalia jambo hilo. Ninawatakeni mliandike, ili mweze kuisoma.

Hawakuwa farasi wa kawaida. Walipumua moto, nao walikuwa na dirii za yaspi, na—na walikuwa na mikia. Na kwenye ncha ya mkia ilionekana kama nyoka, kichwa cha nyoka nchani mwake, akiuma. Mnaona? Ilikuwa ni farasi wa kiroho, pepo wa kiroho, farasi wa vita, ambao walikuwa wamefungwa kwenye Frati miaka hii yote, pepo wasio wa kawaida. Ilikuwa ni kitu gani? Ile Milki ya kale ya Kirumi ikifufuliwa; yale mateso ya Wayahudi. Walikuwa wamefungwa kwa karibu miaka elfu mbili, kwenye mto Frati, hawawezi kuvuka hadi kwenye ahadi; dhehebu la kidini lililokuwa likijaribu kuingia upande ule mwingine. Frati, mwajua, ilipitia Edeni. Lakini walikuwa wamefungwa kule, pepo laki mbili wa mateso.

67 Basi angalia kinachotendeka chini ya hiyo Baragumu ya Sita. Waliachiliwa dhidi ya Wayahudi; mateso ya Wayahudi. Pepo wasio wa kawaida, karibu miaka elfu mbili, halafu wakafunguliwa na Stalin, Hitler, juu ya Wayahudi. Mnasema, "Vema, hiyo si Urumi." Ni roho yule yule. Walifanya mambo yale yale waliyowafanyia Wakristo, katika siku za kale za kipagani za Kirumi. Sasa angalia Israeli ya kawaida, na Kanisa la kiroho sasa, tunapoitenganisha hapa. Akawaachilia Wayahudi.

Mnakumbuka, chini ya Muhuri wa Sita, jinsi kila mmoja wa wale wafia imani, kulingana—kulingana na Neno la Mungu, wanavyopokea nguo ndefu. Walipewa hizo kwa neema, kwa maana wao walipofushwa wasiweze kuiona Injili yao, kusudi watu hawa wapate kuitwa kutoka kwa Mataifa kwa ajili ya—ya Bibi-arusi. Walipewa nguo ndefu, Biblia inasema hapa, chini ya hiyo Baragumu. Hao Wayahudi, ambao wanampinga Kristo kabisa na kila kitu; sababu ya kufanya hivyo, ni kwa sababu Biblia ilisema wamepofushwa. Nao walipofushwa kwa ajili yenu. Na Mungu mwenye haki anajua ya kwamba wangeipokea Hiyo, bali walifanywa vipofu kwa ajili yenu. Biblia ilisema hivyo.

68 Huo hapo ule ufalme wa Kirumi, uliofungwa pale na (nini?) Nguvu za kidini. Ambapo, Rumi, Rumi ya kipagani ilifanyika Rumi ya kipapa, na ilikuwa imefungwa kule katika mapokeo yake ya Kikristo. Ile sehemu ya Kikristo, na—na ushirikina iliyokuwa nao wa Rumi kuweka vitu hivi vyote; kuabudu wanawake, na upuzi huu mwingine wote, na siku za Krismasi, na sikukuu, na siku takatifu, na kadhalika. Imefungwa na

mapokeo hayo ambayo haiwezi kuachilia, kwa sababu ni kinyume cha kanuni za Kikristo. Bado ni roho yule yule wa kikafiri, roho wa kipagani! Na hiyo roho iliingia katika mataifa ya ulimwengu, kulingana na unabii wa Ezekieli na hao wengine.

Nao walifunguliwa juu ya Wayahudi, wasiojua kitu juu ya Roho. Hizo hapo siri zako ambazo zimefichwa chini ya Muhuri huo pale. Mnaona? Angalia jambo hilo. Tulipitia hayo. Nami nitawaonyesha Baragumu hii hapa, hii Baragumu ya mwisho, kile kinachotukia. Hao hapo. Hizi Baragumu zinafunguliwa juu ya Wayahudi, (hamwoni?) Si kwa Mataifa. Mataifa, wakati Mihuri hiyo ilipofunguliwa, wametiwa muhuri; wakati umekwisha; Kanisa limeitwa.

69 Mnakumbuka lile ono juzijuzi? Mnakumbuka kule ku-…kule kuonekana kwake hapo kabla? Ni wangapi wanaokumbuka, Jumapili iliyopita? Jinsi lilikuwa pale sawasawa kabisa, likapita pale. Tuliliona, kabisa, tukaona kitu hicho kichafu na chenye vinyaa kikijitokeza, kinachojiita kanisa, upotovu wa mwisho. Kisha maskini Bibi-Arusi huyo, wa kila taifa, kila mmoja wao amevalia kama taifa walimotoka, wakitembea tu mbele za Bwana kikamilifu.

Mnaona, kutakuwako na wakati, wakati mwingine, ambapo watasema, "Vema, nilifikiri Kanisa lilipaswa kuondoka kabla ya mateso. Nilidhani kulikuwa na Kunyakuliwa."

"Tayari umepita wala hukujua."

Hivyo ndivyo alivyosema kumhusu Yohana wakati mmoja, mwajua.

Kasema, "Vipi, mbona manabii wanasema ya kwamba … waandishi, ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?"

Yeye alisema, "Yeye tayari amekuja." Na hata wanafunzi hawakujua jambo hilo. "Walimfanyia yale waliyoorodhesha."

Unyakuo utakuwa vivyo hivyo. Katika—katika saa moja … Yeye aliahidi kufanya hivyo. Yeye hakuahidi kumwonyesha Eliya namna hiyo, bali aliahidi kumchukua Bibi-arusi namna hiyo. "Katika saa usiyowazia," badiliko tu, katika muda wa kufumba na kufumbua jicho, atanyakuliwa. Ndipo unaachwa, basi huo ndio wakati!

70 Miaka elfu mbili, roho hii kupitia kwa watu wa Kirumi, kanisa la Kirumi, haikuweza kusogea. Bali roho iyo hiyo ikijitokeza, kwanza, kule chini ikamwingia Mussolini huko Rumi, yule dikteta. Mnajua hao watano …

Mambo saba aliyonionyesha, mnamo mwaka wa '33, yangetimia. Matano ya hayo tayari yamepita. Daktari Lee Vayle anaandika kitabu juu yake sasa. Mnaona? Mambo matano, kikamilifu, na kuna mambo mawili tu yatakayotukia. Kasema, "Ingetukia kabla tu ya kule Kuja." Hapa tuko kwenye mwisho sasa, na inaonekana kama jambo hilo la sita linasogea moja kwa moja. Mnaona? Kikamilifu, hasa, hata vile vita na jinsi vingetukia, sawasawa kabisa kwenye alama, na hakuna hata wakati mmoja lilikosea.

Sikilizeni, enyi watu, tunapaswa kuhesabu kila saa. Hujui tunasimama wapi. Karibu sana!

71 Naam, sasa alifungulia, juu ya, chini ya Muhuri ile ya Sita, pepo hawa wa kiroho laki mbili, walianzia kule Rumi, Ujerumani, Hitler. Na angalia katika Biblia, ambapo walipokea, kamwe … Walipokea nguvu kama wafalme, bali hawakutiwa taji. Dikteta si mfalme aliyevikwa taji; pokea tu nguvu kama mfalme.

Loo, Roho wa Mungu akitenda kazi kupitia kwangu sasa, mwajua, akisema tu jambo fulani. Sijui jinsi ya kulisema, wala niseme nini, na labda afadhali nisiliseme.

72 Angalia, elfu mbili- … pepo elfu mia mbili waliwafungulia Wayahudi hao, walipowachoma moto, waliwasulubisha. Wanaweka povu katika mishipa yao ya damu. Waliwaua, hata hawakuwa na gesi zaidi ya kuwaulia. Nao wakawapiga risasi, hata hawakuwa na risasi zaidi za kuwapiga. Nao—nao walifanya kila kitu wangeweza kufanya. Waliichoma miili yao, na kila kitu; na kutundikwa kwenye ua, watoto na wote, watu wasio na hatia. Kwa sababu walikuwa Wayahudi, walifanywa hivyo. Bali Mungu alisema alimpa kila mmoja wao nguo ndefu, ingawa hawakuzistahili, bali neema Yake ya kuwapofusha kusudi tupate kuona.

Ile Muhuri ya Saba bado haijafunguliwa, mwajua. Huko ndiko kuja Kwake.

73 Kwa hiyo wakati wangali chini kule, lakini, Yeye anatuonyesha hapa, kabla ya kutukia. Kama vile Yohana, Yeye alimpandisha juu.

Na wakati mmoja, tukitembea juu ya bahari, mwajua; akasema, "Vipi kuhusu mtu huyu anayeegemea kifuani Mwako?"

Yeye akasema, "Imekupasaje wewe kama akikaa hata nijapo?" Mnaona, yeye hakukaa, bali alimchukua na kumwonyesha jambo hilo, jambo linalotukia mpaka Yeye atakapokuja. Alimwonyesha tu, akamwonyesha Yohana mpango wote.

74 Angalia, tunaona sasa ya kwamba mamlaka yale ya asili chini ninii ya asili, kwa taifa la asili, Israeli, yalifunguliwa pale. Nayo yalifanya kitu gani? Yaliondoka yakaenda yakafanya vita, na jinsi lilivyoua na kutesa.

Sasa katika milki yake ya kidini! Mimi…hivi ninyi…

Natumaini ya kwamba Mungu atayafungua macho yenu kwa jambo hili sasa. Maana, natambua ya kwamba huku si kuzungumzia tu kanisa hili hapa. Kanda hii inaenea kote ulimwenguni. Wala simaanishi kumdhuru mtu ye yote, bali ni kusema Kweli tu.

Sasa milki ya kidini imefunguliwa, kutoka kwa ufufuo wa kawaida wa Rumi ya kipagani, ikawaendea hao Wayahudi, ambao daima imekuwa adui wao. Yule simba, mwenye meno na kila kitu, aliwapondaponda na kuwavunjavunja hao watu. Rumi, daima imekuwa adui wa Mungu! Nao ulifunguliwa katika roho yule yule, na watawala wa mabavu wa ulimwengu, kwa maana huo utaratibu wa kidini ulikuwa ungali unashikilia. Sasa umefunguliwa.

75 Imefanya nini? Katika "ujanja," kama Yeye alivyosema, itakuja kama kujipendekeza. Naye amefanya nini? Yeye analeta Baraza la Ekumeni la Kiprotestanti la Makanisa ya Ulimwengu, roho wa mpinga Kristo juu ya wote wawili, akiwaleta machinjoni, kama walivyowafanya wale wengine, katika saa ya kumwita Bibi-arusi. Vipi? Amefunguliwa katika roho ya kanisa. Wakafunguliwa juu ya nini? Si juu ya madhehebu; juu ya Bibi-arusi! Lakini hapa utalipata, Bibi-arusi hatapitia wakati huo. Biblia inasema la. Kanisa litafanya hivyo, bali si Bibi-arusi. Hivi hamwezi kuona? Wahudumu, hivi hamwezi kuona jambo hilo, ndugu?

Unasema, "Kanisa halina budi kupitia kwenye mateso, kwa ajili ya—kwa ajili ya ukamilifu Wake." Damu ya Yesu Kristo inamkamilisha Bibi-arusi.

Mtu anayemchagua mke hampitishi katika mateso mengi; yeye tayari amepata neema, pia, pamoja naye; amepata neema kwake. Yeye—yeye humchumbia. Na, kama kuna jambo lo lote, atamzuia kutoka kila mahali kugeuza mkono wake. Neema Yake ni kuu sana juu yao.

76 Na ndivyo itakavyokuwa juu ya Bibi-arusi, na ndivyo itakavyokuwa juu ya Bibi-arusi. Sisi ni viumbe wasiostahili, wanaostahili kuzimu, bali neema Yake inatushikilia kupitia humo. Angalia ni wangapi waliopotea na ni vipofu! Ni wangapi, ni wenye dhambi wangapi waliokuwepo ulimwenguni, ile saa niliyookolewa! Mungu aliniokoa kwa kusudi fulani; nami nimedhamiria, kwa mapenzi Yake, kufanya kusudi hilo. Sijali ni kitu gani kingine kinachoendelea; Ninataka kufanya hivyo.

Na katika saa ninapoona makanisa yote, madaha yao makuu, "na tajiri, na hatuna haja ya kitu," wanasema; na kuwaona, wenye mashaka, wanyonge, vipofu; halafu wanakupigapiga mabegani, wanakutaka upatane nao. Nilizaliwa kwa kusudi fulani, hilo ni kukilaani kitu hicho na kuwaita watoke. Hili nalifanya.

Kumbukeni, wakati Yesu alipokuja duniani, hakukuweko na mtu mmoja kwa mia duniani aliyejua ya kwamba Yeye alikuwa hapa. Yeye alikuja kuchukua kundi hilo lililoteuliwa. Kasema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na yote aliyonipa," wakati uliopita, "Baba, watakuja. Watajua jambo hilo. Watalisikia."

77 Angalia kule kufunguliwa kwa roho hii ya kidini. Sasa miaka ishirini baadaye, baada ya vita hivyo, tunaona kule kufunguliwa kwa roho ya kidini. Chini ya nini? Muhuri wa Saba; ile Baragumu ya Saba kwa Wayahudi.

Angalia mwezi ukiingia giza. Chini ya nini? Angalieni ukichorwa, Mwana wa Adamu akifukuzwa kanisani.

Ni kitu gani? Kujiunga na kundi la kidini. Mwe—mwenendo wa kidini, na pamoja na Baraza la Makanisa Ulimwenguni, limemwingiza kila mtu… Kitu hicho kinawakilisha nini? Naam, huna budi kuacha mafundisho yako yote ya kiinjilisti na kadhalika. "Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipopatana?" Hawawezi. Yesu alisema hawawezi. Na kanisa linawezaje, Wamethodisti na Wabatisti kutembea pamoja? Kanisa la Kristo linawezaje kutembea na Wapresbiteri? Mkatoliki anawezaje kutembea na Mprotestanti? Mprotestanti anawezaje kutembea na Mprotestanti?

Lakini Bibi-arusi anaweza kutembea pamoja na Neno, ambalo ni Kristo. Lazima iwe katika makubaliano. Si utaratibu wa kidini; bali ni Neno. Huna budi kukubaliana na Neno, kutembea pamoja na Neno. Yesu alisema hivyo. Hilo linafanya jambo hilo kuwa sahihi.

78 Angalia, huyo hapo sasa. Yeye amefunguliwa, kuita ncha hizi zote zilizolegea, "Loo, vema, haileti tofauti yo yote, hata hivyo."

Hivyo ndivyo Shetani alivyomwambia Hawa, "Haileti tofauti yoyote. Ni sawa. Hakika, Mungu ni Mungu mwema. Yeye anatupenda sisi sote." Yeye hafanyi hivyo.

Unasikia mengi sana juu Yake kuwa ni Mungu mwema. Yeye ni Mungu mwema, lakini, akiwa mwema, hana budi kuwa mwenye haki. Hakuna wema bila haki. Hakuna haki bila sheria, bila adhabu, hukumu. Kwa hiyo tuko katika saa hiyo, tunayoishi.

79 Angalia, upesi sasa, hawa pepo wasio wa kawaida. Basi, chini ya—chini ya himaya ya Umoja wa Mataifa, makundi yaliyoungana pamoja, Mashariki na Magharibi.

Sawasawa tu na mguu wa kulia na mguu wa kushoto wa ile sanamu aliyoona Danieli, jinsi wasingekubaliana na kuchanganyikana pamoja. Na neno Eisenhower, katika wakati huo … *Eisenhower* maana yake ni "chuma." *Khrushchev* maana yake ni "udongo." Naye alitoa kiatu chake na kukipigisha [Ndugu Branham anapigapiga kwenye mimbara—Mh.] dawati kwenye…wakati Baraza la Mataifa, ama U… kwenye UM. Khrushchev alifanya jambo hilo, akikung'uta vumbi lile… Loo, jamani! Saa tunayoishi! Kanisa na hali yake!

Lakini, Mungu ashukuriwe, yule Bibi-arusi mdogo amejifanya tayari. Haitachukua muda mrefu. Shikilia tu. Haitachukua muda mrefu. Sijui ni muda gani, sijui ni lini; hakuna mtu anayejua jambo hilo. Lakini tunajua umekaribia sasa, halisi.

80 Angalia dini. Angalia jambo hilo, la kawaida, jinsi lilivyowafanyia hao Wayahudi. Hao walikuwa ni watu walioshikilia sheria za Mungu. Haidhuru ni makanisa mangapi yanayoinuka, chochote kile, walipofushwa wasimtambue Kristo, nao wakashikilia hiyo torati. Ndipo Mungu akawapa nguo ndefu, kila mmoja wao, maana walishuka wakafia imani. Mnaona? Wao ni—wao ni … Walipofushwa kwa ajili yetu.

Hapa sasa, Kanisa, ambalo halijui kitu ila Biblia. Bila kujali utaratibu wa kidini, madhehebu, hawajui kitu kuhusu hayo. Yote ni mageni kwao. Wanamjua Yeye, na Yeye pekee.

81 Watu siku hizi wako kwa namna fulani kama Petro na hao wengine walivyokuwa, kule juu kwenye Mlima wa Kugeuzwa. Waliingiwa na shauku wakati walipoona ya kimbinguni yakitendeka, na mmoja akasema, "Tutaunda kanisa moja la—la manabii, na moja la Musa."

Na hivyo ndivyo watu, Wapentekoste walivyofanya. Wao walisema, "Tutaunda moja, Assembly of God; na lingine, church of God; na lingine, Umoja; na lingine, Uwili," na kadhalika namna hiyo.

Bali alipokuwa katika kusema, Yehova alipaza sauti, "Huyu ni Mwanangu mpendwa," Ambaye ni Neno, "msikieni Yeye!" Mnaona? Yeye ni Neno.

82 Saa tunayoishi, mambo ya kidini, mambo ya roho zikiungana pamoja sasa na kuwaleta kwenye maangamizi haya makuu, kufutilia mbali. Tayari imeandikwa hapa, katika taifa hili sasa, ya kwamba makanisa haya hayana budi kufungwa isipokuwa uwe pamoja na madhehebu. Ni muungano, ni kususia, kama tu alama ya mnyama.

Na sasa mnaona yule mnyama ni nini, sivyo? Ni mamlaka. Na mamlaka, mamlaka ya kidini, Yesu alisema, "Yangefanana sana na kitu kilicho halisi, hata yangewapoteza walio Wateule kama yamkini." Lakini Yeye aliahidi kuwa na kitu fulani hapa kwa ajili yetu katika siku hiyo, ili kwamba tusidanganywe, na hilo ni Neno, na Kristo kulidhihirisha kwetu. Hao ni wasio wa kawaida, pepo, hawaonekani kwa macho, bali unaweza kuona wanayofanya. Mnaona?

83 Angalia, wakati kundi hilo linapopanda farasi, wakijifanya tayari kukanyaga kila kitu ambacho hakitakubaliana nao, kuna kundi lingine linaloandaliwa, baada ya kitambo kidogo, Ufunuo 19. Mara ya pili Kanisa linaposikiwa, linakuja, pia, si katika farasi hasa, bali Biblia ilisema, "Yeye alikuwa amepanda farasi mweupe, na majeshi ya Mbinguni yalikuwa yakimfuata juu ya farasi weupe." Hiyo ni kweli?

Wakati kundi hili hapa lina elfu mbili waliofungwa kwenye mto Frati, nao walikuwa wamefungwa kwa miaka elfu mbili, pia kanisa hilo limemfunga Roho Mtakatifu kwa karibu miaka elfu mbili, chini ya ufia dini kule nyuma, na chini ya nyakati za kanisa. Amefungwa, si kwenye mto Frati, bali kwenye milango ya kanuni za imani na mafundisho ya sharti, hata Roho Mtakatifu hawezi kufanya kazi kanisani kwa sababu ya taratibu zilizobuniwa na mwanadamu. Bali atawekwa huru, Bibi-arusi anarudi, hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Na hao wawili wanakutana kwenye uwanja wa vita, Lusifa na Mikaeli tena, kama hapo mwanzo. Wamefungwa kwa miaka elfu mbili, karibu, karibu miaka elfu mbili.

84 Si elfu mbili hasa, maana Warumi waliendelea kusonga mbele, Tito mnamo A.D. 96, na kuendelea hivyo, wakawaua Wayahudi. Warumi! Ni nani aliyewaua Wayahudi? Tito alikuwa nani? Jemadari wa Kirumi. Damu ilitiririka kutoka malangoni na kutelemka kule, hata kwenye…loo, wakawaua, wanawake, watoto, na kila kitu. Hivi Ezekieli 9 haikusema wangefanya hivyo? "Pita katikakati ya mji ukatie alama juu ya watu wanaougua na kulia," Ro—Roho Mtakatifu. Na hao wengine "yule mtu mwenye kuua akatokea," ambaye alikuwa amefungwa; akawashikilia, akawashikilia, hata wakaondoka wakaenda na kuua kila kitu kilichokuwa mle ndani. Wasichana, wanawake, watoto, watoto wachanga, na cho chote kile, wote walivawa. Kweli kabisa.

Hili hapa tena, likijirudia lenyewe. Na huu hapa ule mfumo wa kidini ukirudi moja kwa moja, ukififia, ukikanyaga kila kitu kinachoitwa Mungu. Loo, wao wana utaratibu wao, na mashirika, na madhehebu, bali hayo hayana uhusiano wo wote na Biblia. Watakuambia upesi hata hawaiamini. Naam, bwana. "Sema yale kanisa lisemayo."

85 Ni yale Mungu asemayo! Hilo ni Neno. Bibi-arusi yuko pamoja na Maneno; wao ni Mmoja. Wanawezaje kuwa Mmoja? Wakati Neno hilo, ambalo limeandikwa mle, linakuwa ndani yako, na kukufanya—kukufanya wewe na Neno kuwa Mmoja. Hivyo ndivyo hasa alivyoahidi.

Halafu, Hilo linafasiri. Mungu hahitaji mfasiri. Wanasema, "Vema, tunalifasiri namna hii." Huna haki ya kufasiri chochote. Mungu hujifasiria Mwenyewe. Mungu alisema, "Iwe nuru," na ikawa nuru. Ni nani anayefasiri jambo hilo? Yeye alisema, "Bikira atachukua mimba," naye akachukua mimba. Hilo halihitaji mfasiri yeyote; tayari imefasiriwa. Mungu alisema mambo haya yangetukia katika siku hii, na yanatukia. Halihitaji kufasiriwa. Linajifasiri Lenyewe. Loo, jamani!

86 Ufunuo 9:1, chini ya Baragumu ya Tano, mfalme wao … Angalia, Ufunuo 9:1 sasa, mfalme wa kundi hili kubwa la farasi laki mbili. Walikuwa na mfalme juu yao, na, kama tukiangalia, ilikuwa ni nyota iliyoanguka. "Kwa nini umeanguka kutoka mbinguni, Ee Lusifa?" Loo, jinsi Daktari Smith alivyochanganyikiwa na hayo huko juu, lakini, ni sawa, mnaona, hayakuwa kwa ajili ya wakati wake. Mnaona? Vema. "Alikuwa wa kuzimu; mfalme wao alikuwa mfalme wa kuzimu."

Ufunuo 17:8. Niliandika jambo fulani hapa chini. Nitasoma tu. Mnaona hapa, Ufunuo 17:8. Nataka kuona yale inayosema hapa, maana sijui namna ya kuligusia jambo hili linalofuata, 17:8.

> *Yule mnyama uliyemwona alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari kupanda kutoka kuzimu na kwenda kwenye uharibifu. Na hao wakaao juu ya nchi, wasioandikwa majina yao katika kitabu cha—-cha uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, watastaajabu* wamwonapo *yule mnyama, ya kwamba alikuwako, naye hayuko, naye atakuwako.*

Mnaona, "alikuwako," papa moja anakufa, mwingine anatawazwa. "Mnyama aliyekuwako, naye hayuko, ambaye yuko; naye hayuko, ambaye yuko." Habadilishi utaratibu wake; ni papa, wakati ule ule, kila kitu. Kila kitu hakina budi kuingia katika utaratibu ule ule.

87 Na itakuja wapi? "Hata kuzimu." Na Biblia ilisema hapa, ya kwamba, "Kiongozi wa jamaa hawa alitoka kuzimu, na huyo alikuwa ndiye mfalme wao," naye anaketi na taji lenye sehemu tatu, na anawaunganisha Waprotestanti pamoja naye.

Nilimsikia kasisi wa Kiluteri akisema, juzijuzi, kasema…ama, muhubiri wa Kiluteri, kasema, "Vema, watu huniuliza kwa nini mimi huvaa u—ukosi. Wanawezaje kunitofautisha na…" Ulikuwepo kule? [Ndugu fulani anasema, "Ndiyo." — Mh.] Naam. Na, huo, huo si ulikuwa ni upuzi? Ka—karibu nijisikie kama kutapika, nikaondoka pale jukwaani. Wao wakasema, "Kwa kuwa, hakupaswi kuwa na tofauti yo yote."

Kama Luther, Martini Luther, angalisikia jambo hilo, angegeuka upande mwingine kaburini mwake, aseme, "Enyi wanafiki, nyinyi hamhusiki katika hadhi yangu." A-ha. Mnaona?

Lakini mnajua mahali ilipofikia? "Hakuna tofauti."

88 Kuna tofauti. Hata kuna kutofautiana kwa kibinafsi. Mungu alisema, "Nitengeeni Mimi, na Paulo na Barnaba," hiyo ni kweli, "kwa ajili ya kazi." Jitengeni! Mungu ni mtenganishaji, si mchanganyishi. Mtengani- … Kanisa linataka mchanganyishaji bora, leo, ambaye anaweza kuwaruhusu kuvalia nguo za kuogelea, na kaptura, na cho chote kile, na kutoka nje na kufanya yasiyofaa namna hii. Lakini Mungu alisema, "Nitengeeni Mimi!" Jitenge mwenyewe na ulimwengu!

89 Ufunuo, tunaona hapa, ya kwamba, "mfalme wao alitoka kuzimu," na yeye yule ambaye "alienda kuzimuni," kuingia na kutoka, kuingia na kutoka, akatoka.

Angalia katika Mambo ya Walawi, mlango wa 23, jinsi tafsiri ilivyo kamilifu pamoja na utaratibu wa Neno, kwa yale tunayojaribu kutoa sasa. Angalia jambo hili sasa, ule utaratibu. Sasa tunaona. Hebu na tufungue tu na kusoma hayo kwa muda kidogo tu. Katika Mhu-…si Mhubiri, bali Mambo ya Walawi. Mambo ya Walawi 23, sasa angalia jambo hili hapa, Mambo ya Walawi sura ya 23 sasa. Nasi hatutaki kukosa jambo hili hata kidogo, sasa, ili tuweze kulipata hasa jinsi Bwana alivyoandika hapa kwa ajili yetu. Hakika siwezi kupata Mambo ya Walawi katika Kutoka, sivyo? Vema, Mambo ya Walawi sasa. "Na Bwana …" 23.

> *…BWANA akanena na Musa, na kumwambia, Nena na wana wa Israeli, uwaambie, Mwezi wa saba, siku ya kwanza ya mwezi, kutakuwa na kustarehe kabisa kwenu, ni ukumbusho wa kuzipiga baragumu, na kusanyiko takatifu.*

Mnaona?

> *Mtafanya…ile kazi ya utumishi; nanyi hamtasongeza…sadaka kwa BWANA kwa njia ya*

*moto.*

*… Nanyi mtasongeza sadaka kwa BWANA kwa njia ya moto.*

Sasa angalia. Sasa angalia.

*Kisha BWANA akanena…Musa, na kumwambia,*

*Lakini siku ya kumi ya mwezi huo wa saba ni siku ya upatanisho;…*

90 Mnaona, ule upatanisho ulifuata ile … Angalia sasa. Upatanisho ulifuata sauti ya baragumu. Mnaona? Ni nzuri iliyoje! Mnaona? Siku ya upatanisho ilifuata baragumu.

Sasa—sasa, zile siku hamsini za baragumu, kwetu sisi, zinawakilisha kwa mfano wakati baragumu ilipopigwa kwenye pentekoste, ambayo ilikuwa siku hamsini. Sasa—sasa—sasa, baada ya jambo hili, Wayahudi walikataa Hilo.

Sasa zile Baragumu ni kuwaita warudi kwenye ule Upatanisho, mnaona, ule Upatanisho walioukataa. Nao walikataa kusudi macho yetu yapate kufunguliwa; yao yalikuwa yamefungwa. Na katika wakati huu, Mihuri hii ilifunguliwa, na zile—zile—zile Baragumu zikapigwa. Na sasa, katika kupigwa kwa Baragumu, kabla tu ya Masihi kuja, maana hawana budi kuwa katika Palestina. Na mnakumbuka Mungu aliufanya mgumu moyo wa Farao, apate kuwafukuza kutoka Misri; naye akawafanya wagumu akina Stalin, Mussolini, na wote hao, apate kuwarudisha kwenye nchi ya ahadi, mahali ambapo wale mia na arobaini na nne elfu wanapaswa kuwa.

Na sasa, kwa mara ya kwanza kwa maelfu ya miaka, miaka elfu mbili na mia tano, kwamba Israeli ni taifa lenye bendera yake, jeshi lake, na yote, na linahesabiwa katika—katika UN. Mara ya kwanza imekuwa hivyo. Bendera ya kale sana iliyopata kupepea duniani, wakati huu, inapepea tena, zile ninii tano…nyota yenye ncha tano ya Daudi. Yeye alisema angeinua ile bendera katika siku za mwisho, wakati watakaporudi. Tuko mwishoni. Hakuna shaka juu yake. Tuko hapa.

91 Angalia sasa, upesi, Ufunuo 9, chini ya ile baragumu saba, "mfalme wao ametoka kuzimu."

Halafu katika Mambo ya Walawi, sasa, jinsi tafsiri ilivyo kamilifu hapa pamoja na Neno! Kwa sababu, mnaona, mara baadaye, yubile ya pentekoste ilifuata ile siku ya upatanisho; ule utaratibu wa wakati wa sikukuu. Katikati ya sikukuu ya pentekoste, hadi kwenye ule upatanisho, mlio wa baragumu kwa ajili ya upatanisho, ulikuwa ni sikukuu ya pentekoste, kipindi kirefu cha wakati. Angalia, kulikuweko na kipindi kirefu cha wakati kati ya sikukuu ya pentekoste, na kule kuitwa kwa—kwa bara-…kule kupigwa kwa baragumu, zi—zile baragumu kupigwa; kipindi kirefu cha wakati. Kwa kweli, ilikuwa ni siku hamsini, kutoka—kutoka—kutoka kwenye sikukuu ya pentekoste hadi kwenye sikukuu ya upatanisho, ilikuwa ni siku hamsini. Sasa, siku hamsini ni sabato saba hasa.

92 Na sabato saba ni ile miaka saba ya kanisa, Nyakati za Kanisa. Mmelipata? Mnaona? Mnaona? Sasa, Wayahudi wamepofushwa, wakingojea wakati huu wote, wakati malimbuko ya pentekoste yamemwagwa juu ya Kanisa. Nasi tumepitia kwenye nyakati za wafia imani, na kupitia katika nyakati za watengenezaji, na sasa katika wakati wa kuitwa; sehemu tatu, Roho yule yule; kama vile Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Yeye yule. Mnaona? Lakini, Nyakati Saba za Kanisa, zikiwa ni sabato saba.

Sabato saba hasa kutoka—kutoka kwenye tarumbeta ya yubile ya pentekoste … sikukuu ya yubile ya pentekoste, mpaka … Kutikiswa kwa mganda, na halafu yubile ya pentekoste. Na halafu kutoka kwenye yubile hadi kwenye ule upatanisho ni sabato saba, siku hamsini, na mwishoni mwa zile siku hamsini ni u—upatanisho unafanywa. Mnalipata? Sasa, na hii imekuwa ni mfano, ya kwamba Kanisa …

93 Wakati alipofunuliwa, Yeye Mwenyewe, kama Mwana wa Mungu, amekuwa akilifunua Kanisa katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, kote katika nyakati, katika—katika wakati wa kipentekoste, mnaona. Endeleeni tu kupata zaidi na zaidi; kuhesabiwa haki chini ya Luther, kutakaswa chini ya Wesley, ubatizo wa Roho Mtakatifu.

94 Sasa huu hapa wakati wa kuitwa kutoka. Kwenye ule Muhuri wa Sita, wakati u—ulipofunguliwa, mateso yaliwapata Wayahudi, katika mtazamo halisi; na hapa inakuja mateso kwa kanisa, katika msimamo wa kikanisa; kwa sababu, Bibi-arusi tayari ameitwa. Sabato zimekwisha, na ziko tayari kwa Wayahudi kuitwa. Waende wapi? Sikukuu ya Upatanisho. Loo, enyi kanisa, hivi hamwoni jambo hilo? Umeitwa kwenye sikukuu ya Upatanisho, (nini?) Kutambua Upatanisho; si kuku tena na bata bukini, na yale wamekuwa wakifanya. "Mwana-Kondoo wa Mungu, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu," Israeli watajua jambo Hilo.

95 Angalia, hili hapa jambo kuu. Angalia! Loo, jamani! Roho Mtakatifu amefungwa na madhehebu, miaka hii yote elfu mbili. Tunaona kwamba, amefungwa. Sasa angalieni zile sabato, sabato saba, hawangeweza kuondoka kabisa. Bi—Biblia ilisema, "Kutakuwako na siku ambayo haitakuwa usiku wala mchana."

“Na Maandiko yote,” Yesu alisema, “hayana budi kutimizwa.” Hiyo ni kweli? Sema, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina”- Mh.]

Nabii alisema, “Kutakuwako na siku ambayo haiwezi kuitwa mchana wala usiku, bali wakati wa jioni itakuwa Nuru.”

Ilikuwa ni kitu gani? Jua lile lile linaloangaza Mashariki ni jua lile lile linaloangaza Magharibi.

Kila wakati jua hilo linapochomoza, na linavuka na kutua, linamaanisha maisha yako. Mtoto mchanga aliyezaliwa, dhaifu, asubuhi. Yapata saa mbili, anaenda shuleni. Saa tano na nusu, ametoka shuleni, ni joto la mchana. Ndipo linaanza kutua, kufikia umri wa miaka hamsini, sitini, sabini, themanini, tisini. Linaketi kule na kufa; kurudi tu kesho yake, na kusema, “Kuna uhai, mauti, kuzikwa, ufufuo.”

96 Na, angalia, ustaarabu umeambatana na jua. Ustaarabu wa kale sana tulio nao ni China. Kila mtu anajua jambo hilo.

Roho Mtakatifu alianguka wapi? Kwenye nchi ya Mashariki, juu ya watu wa Mashariki. Na Injili imesafiri pamoja na jua. Inatoka wapi? Kutoka huko Mashariki, kuingia Ujerumani, kutoka Ujerumani hadi Uingereza … Ikavuka ule mlangobahari mara tatu. Mediterania hadi Ujerumani, kutoka Ujerumani … Kutoka Mediterrania, kutoka Mashariki, ikaingia Ujerumani, kupitia Mediterrania; kutoka Ujerumani, ikavuka Mlangobahari wa Uingereza, ikaingia Uingereza; kutoka Mlangobahari ya Uingereza, ikavuka Pasifiki ikaingia…ama Atlantiki, ikaingia Marekani.

Na sasa iko kwenye Pwani ya Magharibi. Imevuka taifa hili ambalo ililistaarabisha kisha ikavuka, na kuendelea. Usafiri wa ustaarabu; Injili imesafiri pamoja nayo. Kusafiri kwa ustaarabu; Injili imesafiri pamoja nao. Sasa watu ovyo wote wako kwenye Pwani ya Magharibi, kwenye kila kitu ilichookota, kama vile wimbi linavyokuja.

97 Lakini nabii alisema, “Mwana hataangaza siku hii yote; itakuwa siku ya utusitusi.” Wamekuwa na Nuru ya kutosha, kama vile siku halisi ya mvua, wangeweza kujiunga na makanisa, na kumwamini Bwana, na mambo kama hayo. Lakini, yeye alisema, “Wakati wa jioni, mawingu yataondoka, madhehebu yatafifia.” Na Injili ile ile, Neno lile lile lililofanyika mwili, kama alivyoahidi katika Luka 17:33. Injili ile ile, pamoja na jambo lile lile, lingetukia wakati wa jioni, wakati tu vivuli vinapokuwa vichache. Injili ile ile, Kristo yule yule aliyeishi katika mwili kule nyuma mwanzoni, kwa watu wa Mashariki, ataishi tena katika watu wa Magharibi wakati wa mwisho. “Itakuwa Nuru wakati wa jioni.”

“Maandiko yote yamevuviwa,” na hayawezi kutanguka.

98 Siku hizo kubwa hamsini zimepita. Sikukuu ya pentekoste imepita, sabato saba; mpaka zile baragumu, mfano wa Wakati wa Saba wa Kanisa. Kumbuka, kumbuka, ile … chini ya Baragumu ya Sita, Wayahudi … Mnasikiliza? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Chini ya Baragumu ya Sita, Wa—Wapentekoste wanaikataa Biblia; wale—wale vuguvugu, si Wapentekoste tu, wengine wote. Ulimwengu wa kanisa unamkataa Kristo na Yeye anawekwa nje. Na katika Baragumu ile ile … Na Muhuri ule ule, hasa, wakati ulipofunguliwa, kumwonyesha Yesu nje ya kanisa, akijaribu kurudi ndani; wakati huo huo, Baragumu inapigwa kwa ajili ya Wayahudi, na Wayahudi wanautambua Upatanisho. Utukufu! Haleluya! Loo, jamani!

Roho Mtakatifu amefungwa na mito hii ya kimadhehebu, kwa karibu miaka elfu mbili, lakini atafunguliwa wakati wa jioni, na Ujumbe wa wakati wa jioni. Roho Mtakatifu arudi Kanisani tena; Kristo, Mwenyewe, alifunuliwa katika mwili wa kibinadamu, katika wakati wa jioni. Akasema. Yeye aliahidi jambo hilo.

99 Kulikuwa na hatua tatu zake, kama nilivyosema. Wale wafia imani, wakati wa wafia imani, kwa ajili yake; na halafu hatua ya watengenezaji; na sasa ni wakati wa kuitwa kutoka.

Baada ya kumalizika, katika Wakati wa Laodikia, kulingana na Ufunuo 10, siri ya Biblia yote ingejulikana kwa Bibi-arusi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.” — Mh.] Ufunuo 10. Sikilizeni kwa makini sasa. A-ha. Bibi-arusi, ameitwa kwa Neno; Kristo Mwenyewe akimwita Bibi-arusi, akifanya Waebrania 13:8 dhahiri, ya kwamba Yeye ni “yeye yule jana, leo, na hata milele,” anafanya vivyo hivyo, ni yeye yule. “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Mnaona? Luka 22 … Ama, Luka 17:30, na pia Malaki 4, Waebrania 4:12, Maandiko haya yote yaliyoahidiwa, haya yatakuwa kati ya Muhuri wa Sita na wa Saba, na ile Baragumu ya Sita na ya Saba.

100 Sikukuu ya Pentekoste itamalizika katika kipindi cha Baragumu ya Saba, kwa kuwa inayofuata ni Kuja kwa … Muhuri wa Saba, kwa maana inayofuata ni siri ya Kuja kwa Kristo, na, pia, Baragumu ni sauti kwa ajili ya Wayahudi. Baragumu yao ya Sita inalia, na, inapopigwa, inawajulisha Mwana wa Mungu aliyefunuliwa; nusu saa ya nafasi. Kumbukeni, Baragumu zote zinalia kwenye Muhuri huu wa Sita. Muhuri wa Sita unamaliza ile siri, chini ya Muhuri wa Sita, kabla tu ya ule wa Saba kufunguliwa.

101 Angalia, hapa ni Mambo ya Walawi 23:26. Jinsi Maandiko yalivyo katika utaratibu! Baada ya kipindi kirefu cha pentekoste, ambacho Israeli walikataa huko nyuma; Naye aliliita Kanisa la Mataifa litoke, kupitia sikukuu hii ya kipentekoste. Ni wangapi wanafahamu karamu ya pentekoste ni nini? Ni matunda ya … malimbuko ya mavuno, malimbuko ya ufufuo, sikukuu ya pentekoste.

Msikose jambo hili, enyi watu! Na, ninyi mlio kwenye kanda, sikilizeni kwa makini!

Huu umekuwa ni wakati wa sikukuu ya pentekoste. Wayahudi wamenyamaza; waliukataa. Sasa hawana budi kuitwa warudi kwenye ule Upatanisho. Tunajua Upatanisho ulikuwa ni Nani; hawakufanya hivyo. Na Baragumu ikilia, baada ya yubile ya pentekoste, inawaita Wayahudi pamoja. Hivi hamwezi kuona jinsi hiyo Baragumu, ya mateso chini ya Hitler na hao wengine, ilivyolipuliwa? Nao Wayahudi walilazimishwa kukusanyika pamoja, kutimiza Maandiko.

Sasa mmelipata? Wale wote waliofahamu, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Vema. Vema.

102 Angalia hapa katika Mambo ya Walawi, 26 sasa, utaratibu wa Maandiko. Baada ya kipindi kirefu cha pentekoste, ambacho kinaishia katika kuitwa kwa Bibi-arusi, Bibi-arusi anaitwa na mtumishi. Yule aliyekataliwa, baadaye, ajulikane kwa Israeli, sikukuu ya Upatanisho. Angalia, hapa ni sawa na katika Mambo ya Walawi sura ya 16, sasa, wakati alipoamuru sikukuu ya pentekoste … ama sikukuu ya upatanisho, lakini mahali hapa wanaitwa …

Loo, kamilifu iliyoje! Lifahamuni, enyi wahubiri. Mnaona? Msilikose, enyi wahudumu.

Katika sikukuu hii ya pentekoste, ambayo imewakilishwa katika Mambo ya Walawi 23:26, au 23 na 24, ni sikukuu ya maombolezo, si kuchinja, ya sikukuu. Sikukuu ilichinjawa … Upatanisho ulichinjawa, hasa. Upatanisho ulichinjawa. Mambo ya Walawi 16, inakwenda sambamba kabisa nayo. Ni mahali hapa tu, ambapo wanaitwa Israeli kuomboleza dhambi zao. Jinsi lilivyo kamilifu, leo! Si kule kuchinjwa tena kwa Huyo; ambako, Musa alionyesha mfano, kwa kuupiga ule mwamba mara ya pili; haikufanya kazi. Si kuchinja, kwa sikukuu; bali ni kuomboleza, kwa kukataa Upatanisho. Loo, jamani! Hii itakuwa Baragumu; sikukuu, utakataliwa, halafu Masihi wao anajulikana.

103 Angalia, watamjua Masihi wao watakapomwona. Yeye anakuja katika nguvu, wakati huu, Yule waliyemtazamia. Yeye anakuja katika nguvu, kwa ajili ya Bibi-arusi Mmataifa, na Wayahudi watamtambua. Halafu Biblia inasema … Tumemaliza tu kulihubiri hapa, yapata miezi sita iliyopita, ama zaidi. Biblia inasema, wanaposema, "Ulipata wapi hayo majeraha?" Ni wangapi wanaokumbuka Ujumbe? Inua mkono wako. Hakika, ninyi … Mnaona? "Ulipata wapi hayo majeraha?"

Yeye alisema, "Katika nyumba ya rafiki Zangu."

Kumbukeni mimi nikihubiri juu ya—ule wakati ambapo Yakobo alikuwa amewatuma wana wa Israeli kule wachukue vitu hivyo, na chakula na kadhalika, na jinsi Yusufu alivyotenda kama hakuwajua; na jinsi mambo haya yote yalivyoendelea, ndipo akajitambulisha? Mnakumbuka? Nao waliogopa sana, wakaanza kulia. Ni sawa na shida ya Yakobo.

Na hapa tunawaona Wayahudi chini ya mateso; Sijui wanasimama wapi sasa, bali wanarudi.

Na wakati wanapoona Upatanisho ukitokea, Biblia ilisema, "Walipoona jambo hilo," walisema, "wangetenganisha nyumba moja na nyingine, na kulia siku nyingi, kama—kama familia ambayo imepoteza mwana wao wa pekee. 'Ulipata wapi hayo majeraha?'"

Yeye alisema, "Katika nyumba ya rafiki Zangu." Mnaona?

104 Kumbuka, Bibi-arusi tayari yuko Mbinguni; Mke wa Yusufu alikuwa katika jumba la mfalme. Naye Yusufu akaondoa kila kitu kutoka kwake, naye akajitambulisha kwa ndugu zake; mnaona, Mke Wake na watoto wake na hao wengine walikuwa katika jumba la mfalme wakati atakaporudi kujitambulisha kwa Wayahudi. Huo hapo Upatanisho. Hiyo hapo Baragumu yako ya sauti. Hapo ndipo wanaposema, "Loo!" Ni kitu gani? Huo hapo Upatanisho. "Hayo majeraha yametoka wapi?" Huo hapo.

"Katika nyumba ya rafiki Zangu."

Mnakumbuka yale ndugu wa Yusufu waliyosema? Mbona, wao walisema, "Sasa tutauawa, hakika kabisa. Tulifanya hivyo. Tulifanya uovu kama huo."

Yeye akasema, "La, Mungu alifanya jambo hili kusudi aokoe maisha." Mnakumbuka hadithi hiyo, katika Mwanzo? Mnaona? Mnaona? Vivyo hivyo Yeye alifanya jambo hilo namna hii, kuyaokoa maisha ya Mataifa, Bibi-arusi. Kasema, "Niliyapata katika nyumba ya rafiki Yangu; bali usiwe na hasira, mnaona, usijiogope mwenyewe."

105 Wanasema, "Loo, jamani! Hivi kweli tulikosa kumwona? Je! Huo ulikuwa ule Upatanisho, nasi

tumeukosa? Ee Mungu!" Nao wakasema, "Wanajitenga tu, na kuomboleza kwa siku nyingi." Ni kitu gani? Upatanisho; huzuni. Wakati huu, kule kuja kwa kujitambulisha, Upatanisho, si ule upatanisho wa kawaida wa kuchinjwa, kama vile katika Mambo ya Walawi 16. Lakini Mambo ya Walawi 23 ni wakati wa kuomboleza, wa dhambi zao. Na, dhambi zao zilikuwa, waliukataa Huo.

Loo, hivi hamwoni tulipo? Hivi hamwoni ni kwa nini hizo Baragumu hazina maana kwetu? Zote zilipigwa chini ya Muhuri wetu wa Sita. Mnaona sasa ni kwa nini Roho Mtakatifu hangeniruhusu kulinena? Naye Baba wa Mbinguni anajua, pamoja na Biblia hii mbele yangu, hiyo ni Kweli. Sikujua jambo hilo mpaka jana, juzi; chumbani mwangu ambapo Yeye alinifunulia, akaja kwangu na kuzungumza nami. Nikarudi, nikasema, "Mke wangu, nimelipata sasa. Yeye alikutana tu nami mle ndani na kuniambia. Hili hapa, mpenzi." Mnaona? Mnaona, hilo hapo, mnaona, katika upatano mkamilifu tu.

Loo, watu wasio Naye, ingieni upesi! Huenda ikawa ndiyo nafasi ya mwisho utakayoweza kuwa nayo. Hujui ni wakati gani anaweza kuja.

Sikukuu ya baragumu. Biblia yasema, "Wao wangejitenga wenyewe, mmoja kwa mwingine, na kuomba na kuomboleza, kwa maana ni kama mtu aliyepoteza mtoto wao wa kwanza."

106 Angalia, ninataka kusema jambo moja zaidi. Karibu sana sasa; usikose jambo hili. Ni jambo la kushangaza iliyoje! Tangu Ujumbe wa malaika wa saba (mjumbe wa Muhuri wa Saba) katika Ufunuo 10, ulikuwa ni ule Muhuri wa Saba, mpaka zile Baragumu Saba, kati ya hizo nyakati mbili …

Ee Mungu, tunawezaje kusema Hili, kuwafanya watu kuliona?

Ni kati ya hiyo Baragumu ya Sita, na Baragumu ya Sita na … Ile Baragumu ya Sita na Muhuri ya Sita inalia wakati ule ule. Na kati ya Baragumu ya Sita na Baragumu ya Saba, kuna nabii atakayejitokeza mbele ya Mataifa, kuwaita watu warudi kwenye Mafundisho ya asili ya kipentekoste; na hao mashahidi wawili wa Ufunuo 11 wanawatokea Wayahudi, kuwapeleka kwa Yesu, wakati Kanisa linaponyakuliwa. Wote, manabii! Amina! Neno la Bwana haliwezi kutanguka. Halitakuwa dhehebu! Mnaona jambo hilo?

107 Someni katika Kitabu chenu hapa muone kama kwamba katikati ya Baragumu ya Sita na Saba jambo hili halijaingizwa mle ndani, kuwaacha Wayahudi kuitwa watoke katikati ya lile Pigo la Sita na la Saba, tunakuja kwenye wale mia moja na arobaini na nne elfu (mnakumbuka jambo hilo?), ambao walikuwa katikati ya hayo. Mnakumbuka? Kati ya—ya—ya Sita, Muhuri wa Tano na Muhuri ya Sita … Kati ya ule Muhuri wa Sita na ule Muhuri wa Saba, kulikuwako na kuitwa kwa wale mia na arobaini na nne elfu. Mnakumbuka jambo hilo? Sasa hapo ndipo tarumbeta hizi zinapoingia papo hapo, mnaona, na mateso, na farasi wamefunguliwa pale.

Halafu, kati ya jambo hilo, basi kulikuwako na Ujumbe wa malaika wa saba, ambao ulikuwa ukihubiri na kuwahukumu Wapentekoste. Naye Yesu alikwisha kuwekwa nje; hakuna mtu ambaye angeshirikiana naye, amewekwa nje, amekataliwa. Biblia ilisema hivyo. Kwa kuwa, ni Kristo aliyedhihirishwa miongoni mwetu, Yesu miongoni mwetu sote, akidhihirishwa katika usafi wa Neno Lake, akilifanya lijulikane. Na kama hiyo ni …

Hili si jambo la kujitengenezea tu, marafiki. Hii ni BWANA ASEMA HIVI, Maandiko.

108 Na wakati uo huo … Sasa, mara Kanisa hili (Bibi-arusi) limevutwa pamoja, linanyakuliwa; na ile siri ya Muhuri ya Saba, ama Muhuri ya Saba, ile siri ya kuondoka. Nao Wayahudi wanaitwa kwa siri ya Baragumu ya Saba, ambayo ni manabii wawili, Eliya na Musa, nao wanarudi. Na hapo ndipo Wapentekoste wamechanganyikiwa kabisa; wanatazamia jambo fulani litukie; Kanisa limekwisha kuondoka. Na hilo ni kwa Wayahudi.

109 Sasa, ninajisikia akilini mwa mtu fulani, nikisema, "Huyo asingeweza kuwa ni Musa." Naam, ni kweli. Sasa, mnakumbuka, Yeye anaweza kuniambia mawazo yenu. A-ha. A-ha. Ninaendelea kuhisi kwamba … Vema.

Hebu ninyoshe hilo kwa ajili yenu. Ilikuwa ni Musa. Maana, hili hapa wazo lako. Unasema, ya kwamba, "Musa, haingeweza kuwa ni Musa, maana Musa alikufa." Mnafikiri ni Eliya. Ni Eliya, kweli. Wakati, unafikiri, "Ni Henoko." Mnasema, "Musa tayari amekufa." Lakini, kumbuka, angeweza kufufuka tena. Alifanya hivyo. Miaka mia nane baadaye, miaka mia kadha baadaye, yeye alitokea kwenye Mlima wa Kugeuzwa Sura. Unasema, "Baada ya mtu kufa?" Naam, bwana. Lazaro alikuwa amekufa; akafufuka tena; kisha ikambidi afe tena. Mnaona? Hakika. A-ha. Na hata waovu watafufuliwa tena, na halafu itawabidi kufa mauti ya pili. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo ondoa hilo akilini mwako. Ni Musa. Angalia huduma yako, vile vile hasa Musa na Eliya walivyofanya; akafunga mbingu na kuinyunyizia moto. Mnajua ni jambo gani walilofanya.

110 Wazia jambo hilo! Ni wakati wa mwisho, jamani. Haleluya! Siku kuu ya Bwana imekaribia. Kusanyikeni pamoja. Sikukuu ya Masihi; watamkataa Yeye, nao wataona ya kwamba huyo hapo Masihi wao. Biblia ilisema hayo mambo ya ajabu kama haya yangetukia.

Katika Ufunuo 11, wito, huduma yao itakuwa ni huduma ya Musa na Eliya kuwaita Israeli, kutoka kwenye mapokeo ya Kiyahudi; kama tu vile Ujumbe wa malaika wa saba ulivyomwita Bibi-arusi kutoka kwenye mapokeo ya Kipentekoste. Kumbukeni, Musa na Eliya wanapaswa kuwaita Israeli watoke kwenye ule upatanisho wa kale wa mwana-kondoo, na kondoo, na damu, na mbuzi, na sadaka, kwenye ile Dhabihu iliyo hai halisi, kwa Neno.

111 Na Ujumbe wa malaika wa saba, chini ya Baragumu ile ile, kila kitu sawa kabisa, Muhuri ule ule, ni (nini?) Kuwaita watu, Bibi-arusi, kutoka kwenye mapokeo ya Kipentekoste na ya ulimwengu, kwenye Upatanisho halisi, lile Neno, Kristo lililoigizwa. katika Neno Lake hapa, lililofanyika mwili miongoni mwetu. Sayansi imethibitisha jambo hilo, kwa picha. Kanisa linajua jambo hilo, ulimwengu mzima. Tunajua jambo hilo dhahiri, kwa kuwa Yeye hakutuambia kamwe jambo moja katika BWANA ASEMA HIVI ila lile lililokuwa Kweli. Je, Yeye hakusema, kule chini mtoni, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa, vivyo hivyo Ujumbe huu …"

Nimeinua macho yangu, na ni saa sita. Saa ya usiku wa manane imewadia, enyi marafiki, juu yetu. Mnaona jinsi Maandiko yalivyo makamilifu? Kikamilifu, jinsi ilivyokuwa …

112 Hilo, angalia, hilo halitakuwa ni dhehebu fulani kwenda kule na kuwaita Wayahudi. Itakuwa watu wawili, Musa na Eliya. Wote wawili, manabii.

Sasa angalia. Kuwaita Mataifa, Bibi-arusi atoke, Yeye aliahidi katika Malaki 4 kufanya jambo lile lile.

Na Biblia ilisema Yeye angefukuzwa kanisani, katika Wakati wa Saba wa Kanisa. Yeye angefukuzwa kanisani. Litakuwa jeusi kabisa, na liende… Linakuwa jeusi wapi? Linaingia katika mfumo huu wa kikanisa, katika baraza hili la ekumeni, Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Yeye … Yeye ametupwa nje kabisa. Neno Lake, hawawezi kukubaliana Nalo. Mnajua hawawezi. Hata hawawezi kukubaliana katika makundi yao madogo ya wenyeji; watakubalianaje katika jambo Hilo? Kwa hiyo, wanachukua alama nyingine ya mnyama, sanamu ya mnyama. Kumbukeni, Biblia ilisema, "Kulikuwa na sanamu iliyofanywa kwa yule mnyama."

113 Na hii Marekani daima imekuwa namba kumi na tatu. Ilianza na majimbo kumi na matatu, makoloni kumi na matatu; nyota kumi na tatu, milia kumi na mitatu; namba kumi na tatu, na daima ni mwanamke. Anaonekana katika sura ya kumi na tatu ya Ufunuo. Na, kwanza, ni mwana-kondoo; upole, uhuru wa kunena, uhuru wa dini, na kadhalika; na ndipo wanapokea nguvu, na kunena kwa nguvu zote alizokuwa nazo yule joka mbele yake. Ni kitu gani? Joka lilikuwa nini? Rumi. Mnaona, alikuwa na alama, sanamu ya mnyama, kuinuka dhidi ya Kanisa halisi la Mungu. Chini ya hayo madhehebu, watakitesa kitu hiki! Lakini, wanapoanza kufanya hivyo:

Mwana-Kondoo atamchukua Bibi-arusi Wake awe karibu Naye daima,
Jeshi lote la Mbinguni litakusanyika;
Loo, itakuwa tamasha yenye fahari, huku watakatifu wote wamevalia mvazi meupe
yasiyo ya waa;
Na pamoja na Yesu watafanya karamu ya Milele. Amina!
"Njoo ule," Bwana anaita, "Njoo ule." Amina!

Ni siku ya jinsi gani tunayoishi, ile saa! Kimbieni, enyi watu, kimbieni kwa ajili ya maisha yenu!

114 Angalia sasa, katika kufunga, huduma kama malaika wa saba. Hao mashahidi wawili, chini ya Baragumu Saba, kabla tu … ama, Baragumu ya Sita, kabla tu ya ile Baragumu ya Saba kumaliza …

Sasa, kumbukeni, nami niliwaambia ningeirudisha hii, "Baragumu Kuu." Yeye alisema, angefanya nini, hapa katika Isaya? Yeye alisema, katika … "Baragumu Kuu italia. Ile Baragumu Kuu!" Sio Baragumu sasa, sikukuu ya baragumu; kuna wawili wao, Musa na Eliya, kuita ile Baragumu. Lakini, chini ya "Baragumu Kuu," kule Kuja kwa Bwana, kumtangaza Yusufu kurudi, mnaona, kwamba mataifa yote yangekusanyika Yerusalemu. Amina. Mnaona jambo hilo katika Kitabu cha Isaya. Nimewapa tu, muda mfupi uliopita, moja ya hizo sura tulizosoma; hiyo ni katika Isaya 18:1 na 3. Na katika Isaya 27:12 na 13, ndipo Yeye anapopiga hiyo "Baragumu," na mataifa yote yatawatambua Israeli katika nchi ya uenyeji wao, Mungu pamoja naye.

115 Ndipo Bibi-arusi atakuja kuwa pamoja na Bwana Arusi, na Bwana Arusi pamoja na Bibi-arusi; na halafu ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu, baada ya ulimwengu mzima kuangamizwa kwa nguvu za atomiki. Na kutakuwa na "mbingu mpya na nchi mpya," zitaishi milele.

Angalia, moja kwa moja chini ya … Sasa angalia, huduma ya Musa na Eliya itaninii … Sasa, kila mtu analipata? Hebu niseme jambo hilo tena. Huduma ya Musa na Eliya, kati ya Baragumu ya Sita na ya Saba, itakuwa manabii wawili watakao … wao … Israeli daima wanaamini manabii wao.

116 Sasa, kwa nini Roho Mtakatifu aliniambia nilipoanza kwenda kule, kuwaonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, kasema, "bado"? Mnakumbuka jambo hilo, yapata miaka mitano iliyopita, nikienda India? [Kusanyiko linasema, "Amina." — Mh.] Kasema, "Usifanye hivyo."

Nikasema, "Wao walisema, 'Kama huyu ni Masihi, hebu na tumwone akifanya ishara ya nabii. Tunawaamini manabii.'"

Ndugu Lewi Pethrus na hao wengine walinitumia hizo Biblia; wakati walipowapa milioni moja hao Wayahudi wanaotoka Iran na kila mahali, wakirudi, wakikusanyika pamoja, wakawa taifa.

Nikawaza, "Huu ndio wakati wangu." Nilikuwa tayari … Cairo, Misri.

Yeye alisema, "Usifanye hivyo sasa. Saa bado haijafika." Kisha nikarudi nyumbani. A-ha. Loo, jamani!

117 Musa na Eliya hawana budi kuita. Yubile ya pentekoste ingali inaendelea, ama imekuwa mpaka wakati huu. Mnaona? Sasa sikukuu ya Baragumu haina budi kujulikana. Na hii hapa ya Malaki 4 haihusiani na ile pale; hata kidogo, hata kidogo. Angalia, angalia hapa, huduma itakuwa Musa na Eliya, wakibadilisha na kuwaita Israeli kutoka kwenye mapokeo ya Kiyahudi, sikilizeni, kutoka kwenye mapokeo ya Kiyahudi ambayo walikuwa wamechanganyikana nayo. Wakiwa manabii, wataamini—watamwamini, wakiwaita kwenye sikukuu ya Upatanisho, Kristo, wakiwaacha wamtambue Kristo. Watasema, "Yeye yuaja. Yeye atakuwa hapa." Wayahudi watakuwa wakikusanyika, mambo kama hayo.

Na halafu Yeye ajapo, useme, "Mimi hapa." Mnaona?

"Ulipata wapi makovu hayo?"

"Katika nyumba ya rafiki Zangu."

118 Sasa, kama vile wale manabii wawili walivyofanya! Kumbukeni, Bibi-arusi Mmataifa anapaswa kuwa na nabii, anayeitwa Eliya, Eliya, ambaye atawaita watoke kwenye mapokeo yao, Bibi-arusi; ni kama tu vile manabii hawa walivyowaita Wayahudi watoke katika Uyahudi, wakawaingiza kwa Kristo, ule Upatanisho. Na Mataifa tayari wanajua ule Upatanisho, bali ni kumwita Bibi-arusi arudi kwenye Upatanisho wa asili, ambapo hizi sabato (hamsini) wao … Sabato hizi zote saba ambazo wameziacha; kuwaita warudi kwenye wakati wa mwisho. Wale saba … Sikilizeni! Yule mjumbe wa Kanisa la Saba, yule mjumbe wa Baragumu Saba, wote ni manabii. Sasa, hiyo ni kweli.

Walioingizwa, ni wale mia na arobaini na nne elfu.

Kuita, ile Mihuri, ambayo ilikuwa kwa Mataifa. Ilibidi iwe kwa Mataifa, kuwafungulia Mataifa, kuona Kanisa la Mataifa. Hilo tu ndilo tunalojua. Hayo tu ndiyo tutakayosikiliza; yale yaliyokwisha pita. Tunamtazamia Yesu.

Unasema, "Sasa, ngoja kidogo, Ndugu Branham, ninaamini watafanya jambo *hili*."

119 Ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu … Nasi ni Uzao wa kifalme wa Ibrahimu; Bibi-arusi. Ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu alipata kuona kabla ya ishara iliyoahidiwa kuja … mwana aliyeahidiwa kuja, ilikuwa ni nini? Mungu, katika umbo la mwanadamu, ambaye angeweza kuyatambua mawazo ya watu; mtu mmoja, si dazani; mtu mmoja, haidhuru ni waigaji wangapi. Walikuwa na Mmoja, Naye alitambua mawazo yalikuwa mle ndani. Nini? Na, jambo lingine lililotukia, Ibrahimu na Sara wakageuka wakawa kijana mwanamume na mwanamke. Tunajua jambo hilo.

Naam, najua kwa namna fulani hilo linawakaba kidogo. Lakini, kumbuka, ili kwamba tu uwe na hakika ya kujua sasa … Hamsomi Biblia namna hii, mnasoma katikati ya mistari na kuona, kuifanya ile picha ije.

120 Angalia. Sara alikuwa ni mwanamke mzee, Biblia ilisema. Yeye, wao … "Tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa." Hiyo ni kweli? "Uhai wa Ibrahimu ulikuwa umekufa ndani yake, uzao wake." Hiyo ni kweli?

Sasa, kumbukeni, uzao wa Ibrahimu ulikuwa umekufa. Miaka arobaini baadaye alikuwa na wana saba kwa mwanamke mwingine. Yeye alifanya nini? Aliibadilisha miili yao.

Angalia, walifanya safari ya maili mia tatu, wakashuka wakaenda Gerari, safari ndefu sana kwa mzee. Kasema …

Na Sara hata alifikiri wasingeweza kuwa na uhusiano wa kifamilia. Akasema, "Mimi …" Miaka ishirini au zaidi, labda, kabla hawajapata uhusiano wa kifamilia. Kasema, "Mimi ni mwanamke mzee, na bwana wangu, pia; kuwa na furaha tena, kama vijana?"

Akasema, "Kuna jambo lililo gumu kwa Mungu?"

121 Angalia kilichotukia. Mara akageuka akawa msichana mzuri. Akionyesha, mle ndani, akionyesha kile atakachomfanyia Mzao wa kifalme wa Ibrahimu, kumpokea Mwana aliyeahidiwa. Aligeuka akawa kijana …

Angalia, walishuka wakaenda Gerari. Na ni jambo gani lililotukia? Abimeleki, mfalme, alimpenda, akasema, "Yeye ni mzuri na mrembo," naye alikuwa anaenda kumwoa. Hiyo ni kweli? Bibi mzee; na hao wasichana wengine wote wazuri kule. Nyanya, "Yeye ni mrembo. Yeye ni mrembo sana." Mnaona?

Mungu aliubadilisha mwili wake, na akawageuza. Ni siri itakayofunuliwa sasa katika siku hii, na Mwana wa Adamu, mnaona, Ujumbe wa jioni. Mnaona? Akarudi nyuma! Na hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho waliyoona, ilikuwa (nini?) Huo upambanuzi, kabla ya badiliko la mwili kuja.

Na kabla hatujapata kumpokea Mwana, ni jambo gani linalotukia? "Baragumu ya Mungu italia; waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza, mwili mpya; nasi tulio hai na tuliosalia tutabadilishwa, katika dakika moja, kufumba na kufumbua," haleluya,"na tutanyakuliwa pamoja, kumlaki Bwana hewani." Siri imefanywa wazi; ile Mihuri imefunguliwa.

Ile Baragumu ilipigwa kwa ajili ya Israeli; hao manabii wawili wako tayari kuonekana. Ni kitu gani? Kanisa halina budi kuondoka jukwaani sasa hivi, ili waweze kutokea. Yeye hawezi kushughulika na wawili kwa wakati mmoja; Kamwe hakufanya hivyo. Mnaona?

122 Loo, ndugu, angalia! Hakika, kuwaita wote, kuwaita watoke kwenye madhehebu na mapokeo. Sasa tunaona kanisa la wakati wa pentekoste limekwisha.

Bibi-arusi hana budi kuondoka njiani, apate kwenda juu sasa; kusudi wale watumishi wawili, wale watumishi wawili wa Mungu, katika Ufunuo, wale manabii wawili, wapate kujitokeza, kusudi wawapigie ile Baragumu ya Saba, wawajulishe Kristo.

Malaika wa saba, mjumbe, anasema, "Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" Si, "tazama Mmethodisti wangu, Mbaptisti wangu, Mpentekoste wangu." Lakini, "Neno, Mwana wa Mungu, Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu," kwa maana hakuna misingi mingine iliyopo! Mnaona?

Tuna muda gani? Wayahudi wako katika nchi ya uenyeji wao. Bibi-arusi ameitwa. Kimaandiko, kila kitu ni kile hasa alichoahidi. Tuko tayari. Wakati umewadia.

Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu;
Rudini, enyi mliotawanyika, nyumbani kwenu.
Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya mwanadamu inazimia kwa hofu;
Jazweni na Roho wa Mungu, mkazitengeze taa zenu na mzisafishe, Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia!
Manabii wa uongo wanadanganya, Kweli ya Mungu wanaikana,
Ya kwamba Yesu aliye Kristo ndiye Mungu wetu; (hayo ni kweli)
Lakini tutatembea mahali mitume walipokanyaga.
Kwa maana siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya mwanadamu inazimia kwa hofu;
Jazweni na roho, mkazitengeze taa zenu na mzisafishe, (usibahatishe)
Angalia juu, ukombozi wako umekaribia!

123 Nabii alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni."
Itakuwa Nuru wakati wa jioni,
Njia iendayo Utukufuni hakika mtaiona;
Katika njia ya maji ndiko kwenye Nuru leo,
Kuzikwa katika Jina la thamani la Yesu.
Vijana kwa wazee, tubuni dhambi zenu zote,
Roho Mtakatifu hakika ataingia;
Nuru za jioni zimekuja,
Ni kweli kwamba Mungu na Kristo ni Mmoja.

Tuko hapa! Tuko mwishoni. Hilo si jambo la kipumbavu tu la mwanadamu. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

Na tuinamishe vichwa vyetu.

124 Mungu wa rehema, Yehova, Ewe Nwenyezi aliyenguruma kwenye Mlima Sinai; na hao watu wakapiga kelele, "Musa na aseme nasi, wala si Mungu, tusije tukafa." Ulisema, Yehova Mkuu, "Nitawainulia Nabii. Sitasema nao tena namna hii." Lakini Wewe uliahidi kile ungefanya, nawe ukakifanya; Ulitufufua Bwana Yesu. Yeye ni Neno. Ulisema alikuwa hivyo. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili, akakaa kwetu."

Tunaona mambo aliyotutabiria hapa, kupitia nabii Wake, Yohana, kwenye kisiwa cha Patmo. Tunaona likitimizwa, kabisa. Tunaona Roho Mtakatifu akidhihirishwa miongoni mwetu hapa duniani. Tunaona madhehebu yakimtoa kanisani; Neno. Hawana neno dhidi ya watu; ni Neno hilo wanalochukia. Ni kinyume cha mapokeo yao. Kama tu vile ulivyokuwa hapa duniani, Wewe ulikuwa Neno, nawe ulikuwa kinyume na mapokeo yao; nao wakakutupa nje ya makanisa yao, kila mahali.

125 Na sasa, Bwana, hakuna ushirikiano, mahali po pote. Nikijaribu hata kuingia Afrika Kusini, ambako ninajua kuna watu wengine pale ambao bado wanangojea. Kila mahali, na inaonekana kana kwamba hawatanipokea, Bwana. Si kwa sababu yangu, Bwana; ni kwa sababu ya Ujumbe huu. Lakini, Wewe ulisema ingekuwa hivi, nawe umetufahamisha kusudi tusife moyo. Tunajua saa tunayoishi.

Mungu, watu hawa wameketi hapa asubuhi ya leo, katika chumba hiki chenye joto, wakiungua. Wamesikiliza kwa makini. Wanaona sasa, nina hakika. Wasipofanya hivyo, wafunulie, Bwana, kwa nini Wewe usiniruhusu kuchukua hizo Baragumu. Ninaona haina uhusiano wowote nasi. Moja kwa moja kwenye ile Baragumu ya Sita, yote yalitukia, nasi tayari tumeona Muhuri wa Sita ukifunguliwa. Nasi tuliona ono hapa, majuma mawili yaliyopita, juu ya onyesho la awali la Bibi-arusi na kanisa, kama nilivyosema hapa. Kama tu vile ulivyonionyesha, Bwana, nililisema. Tuko hapa. Huenda ikawa imechelewa kuliko tunavyodhania.

126 Ee Baba, kama kuna mtu hapa asubuhi ya leo, ambaye—ambaye amechukua tu ushirikina fulani, ushawishi fulani wa kitheolojia, ama neno fulani la mwanatheolojia ambalo ni kinyume cha Neno la Mungu! Nao hawamjui Kristo halisi, Roho Mtakatifu halisi. Haijafunuliwa kwao, Neno, bado, jinsi Neno litakavyokuwa katika siku hii. Wanaona tu mapokeo. Wao wanaishi katika—katika Nuru inayopofusha. Kama vile wizi mkubwa sana uliopata kufanywa ulimwenguni, ulikuwa Uingereza, ulifanywa kwa nuru ya uongo. Na wizi mkubwa sana kanisa Lako lilipopata kuwa nao, umekuwa wakati walipochukua nuru ya kimadhehebu na kuikataa Nuru halisi ya Biblia, Kristo.

Ee Mungu, turehemu! Waokoe waliopotea, Bwana. Tafadhali, naomba kwa muda kidogo tu zaidi, Yesu. Tuna wapendwa. Muda kidogo tu zaidi. Hivi karibuni Mwamba huo mkuu utakatwa kutoka mlimani. Jalia, Bwana, kama ye yote yuko hapa asubuhi ya leo bila Wewe, jalia waje sasa hivi, kwa utamu, na wakupokee.

127 Huku tumeinamisha vichwa vyetu. Kama ungeinua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Ndugu Branham." Hatuna … Madhabahu na kadhalika yamejaa. Mungu akubariki. Sema tu, "Nikumbuke." Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Ni mamia tu ya mikono kweli!

128 Baba, Mungu, kuna kivuli kidogo mahali fulani. Kiondoe, Bwana. Waliketi hapa katika chumba hiki. Msininii … Huenda Shetani aliyapofusha macho yao, katika nyakati zilizopita, bali naomba ya kwamba Wewe utasamehe jambo hilo, kama ulivyofanya kwetu siku nyingi zilizopita. Lakini sasa kwa kuwa Wewe unatuita sisi sote tuone … Biblia ilisema ya kwamba walikuwa vipofu. Hawakujua jambo hilo. Kasema, "Nakushauri ununue Kwangu dawa ya macho." Mungu, tumia dawa hiyo asubuhi hii juu ya macho yao, wapate kuona. Hata hivyo iwe nyenyekevu, katika kundi la watu wanyenyekevu; na wanyenyekevu, wasio na elimu, na kadhalika, bali hata hivyo hivyo ilivyokuwa hapo mwanzo. Tujalie, Bwana, ya kwamba watampokea sasa hivi. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Mwanao, Yesu.

Nawe ulisema, "Yeye alisikiaye Neno Langu." Nami nina hakika, Bwana, kadiri nijuavyo mimi, wamelisikia. "Na kumwamini Yeye aliyenipeleka," si kujifanya kuamini, bali kuamini kweli, na kuamini yale Neno limesema. "Ana Uzima wa milele, wala hataingia Hukumuni; bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Yohana 5:24.

Tujalie, Bwana, ya kwamba watakuwa Wako, tangu saa hii na kuendelea. Kama kuna msgangao moyoni mwao, uondoa. Kama kuna mtu mgonjwa miongoni mwetu, hebu Roho Mtakatifu mkuu, Bwana, … Ambaye, najua yuko; na akifunua mawazo, akisimama hapa jukwaani. Wanajua yote kuhusu jambo hilo. Ninaomba ya kwamba utawaponya, Bwana. Tuliza maswali yote.

129 Kidimbwi kitafunguliwa kwa wale ambao hawajapata kuzamishwa katika Jina la Yesu Kristo, wakichukua Jina la Bwana Arusi. Wana ule wa kimadhehebu, wa kidini; hakuna mtu aliyepata kubatizwa katika hivyo vyeo vya "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," ama kunyunyiziwa; na mambo hayo ya mapokeo ambayo ni ya makanisa ya wakati huu, mwenendo wa mpinga-Kristo, sanamu ya mnyama. Hakuna mtu aliyewahi kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," mpaka kanisa Katoliki. Biblia yote, na historia yote, baadaye, inasema walibatizwa katika Jina la Yesu.

Paulo alisema, katika Wagalatia 8:1, "Kama Malaika kutoka Mbinguni akija na kuhubiri Injili nyingine yo yote, na alaaniwe." Nawe uliwaamuru hao watu waliokuwa wamebatizwa chini ya Yohana, yeye yule aliyembatiza Yesu, waje wabatizwe tena katika Jina la Yesu Kristo, katika Matendo 19. Kisha akasema, "Hata usimruhusu Malaika kukwambia jambo lingine lo lote."

130 Atakuja mjumbe katika siku ya mwisho, atawaongoza watu warudi kwenye malimbuko, warudi kwenye Imani ya asili. Tujalie, Bwana, ya kwamba yule Mjumbe mkuu miongoni mwetu sasa, yule Kristo mkuu, Roho Mtakatifu alifanya dhahiri, akafanya ufahamu, akilifungua Neno na kutufunulia, jalia awaongoze warudi kwenye Imani asili, ya kipentekoste. Kama vile Petro alivyosema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi." Na ilikuwa hivyo daima, kwa kila mtu, mpaka kanisa la Kirumi huko Nikea.

Mungu, turehemu sasa. Kidimbwi kitakuwa tayari; mioyo inafunguka. Ingia ndani, Bwana Yesu. Tuko katika saa za mwisho. Kama kuna uwezekano, Bwana, wao kuingia katika saa hii; ambao, natumaini na ninaamini ya kwamba upo. Nasi ambao tuko ndani, Bwana, naomba kwamba tujichunguze sasa, ya kwamba tumeiona na kuisikia Sauti ya Mungu ikinena kupitia Neno Lake, nasi tunaijua saa tunayoishi. Tujalie, Baba. Tunawakabidhi Kwako, katika Jina la Mwanao.

Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa.
Kwa upole na upole Yesu anaita,
Anakuita wewe …

www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7